

# YEHOVA-YIRE



...?...kwa kweli ni majaliwa tuliyo nayo, usiku wa leo, kuja katika Uwepo Wako, hilo Jina litoshelezalo kwa yote la Bwana Yesu, Mwanao. Na sasa tunakikaribia Kiti Chako cha neema katika Jina Lake, tukijua ya kwamba Wewe uliahidi kama tungeomba lolote katika Jina Lake, tungelipokea. Tunakuomba uchukue umiliki wetu usiku wa leo, Baba, wa kunena kwetu, kusikia kwetu, ufahamu wetu. Tunaomba ya kwamba utampa baraka kila mmoja ambaye ameingia ndani ya milango hii, usiku wa leo. Utufungie pamoja Nawe, Baba.

<sup>2</sup> Nasi hatujiombei tu hapa, bali rehema kwa ajili ya wale walio wahitaji kote ulimwenguni. Katika huduma za kimishenari, tunafikiri usiku wa leo, katika jengo kubwa la kupendeza kama hili, ambalo tunashukuru kwa ajili yake, watu waliovalia nadhifu, wachangamfu, na waliolishwa vizuri, na kuwazia katika huduma za kimishenari kwamba watu wa Mungu, wasio na jozi ya viatu, wakila sahani moja ya wali kwa juma, wakihubiri Injili. Ee Mungu, ninawaombea watu hao. Saidia, Ee Mungu, ninaomba ya kwamba Wewe utawasaidia, na ni watu hodari.

<sup>3</sup> Tutafanya nini, tunaposoma katika Biblia ambapo walizunguka-zunguka jangwani, nao walikuwa wamevaa ngozi za kondoo na ngozi za mbuzi, walifanywa wahitaji, na hawa wote ambao ulimwengu hata haukuwastahili, basi ushuhuda wetu utakuwaje ukilinganishwa na wao siku hiyo? Baba Mungu, tunaomba ya kwamba utatutikisa kwa Neno Lako usiku wa leo, na kutufanya tujirudie, tupate kuwa mawe hai yaliyowekwa katika Maskani ya Mungu.

<sup>4</sup> Mbariki mchungaji hapa, mashemasi, wadhamini, washiriki wote wa kanisa, na washiriki wa makanisa mengine waliokusanyika usiku wa leo, na wachungaji. Baba, ninaomba ya kwamba sote tutaondoka tukiimba nyimbo moyoni mwetu kwa sababu ya Uwepo Wako. Tunaomba, katika Jina la Mwanao, Mwokozi wetu, Yesu Kristo. Amina.

<sup>5</sup> Ketini. Ninaomba msamaha kwa kuwachelewesha kidogo jana jioni, lakini kwa kuwa ni ibada ya uponyaji, wakati mwingine inachukua tu muda zaidi kidogo. Naye Roho Mtakatifu akianza kutenda kazi miongoni mwa watu, na ndipo ilinibidi kusimama moja kwa moja. . . Inaonekana kana kwamba wakati wewe, ukiwa na ibada wala huiendelezi kwenye. . . Huu kwa namna fulani ni utaratibu tofauti kidogo na yale nimekuwa nikipitia, na kwa hiyo nilizungumza kwa muda mrefu kupita kiasi kujaribu kuwaletea watu somo hilo, wapate kuona kwa ajili ya uponyaji.

Je, mliufurahia Uwepo wa Bwana jana usiku? Yeye—Yeye ni wa ajabu, hakika Yeye ni wa ajabu.

<sup>6</sup> Sasa, usiku wa leo... Nilikuwa nikiwazia jana jioni juu ya Uwepo Wake, na juu ya Uwepo Wake kuponya. Na—na bila shaka, sisi, ungeweza, wakati upako uliposhuka, ungeweza kuwahisi wakosoaji kutoka kila mahali, unajua, bali tunatarajia jambo hilo, mnaona, halina budi kuwapo. Popote wana wa Mungu wamekusanyika pamoja, Shetani ameketi mahali fulani, mnaona, kumbukeni tu. Loo, najua hilo kutokana na ujuzi wa muda mrefu.

<sup>7</sup> Na wakati mwingine unapoifikisha mahali unapopiga vita, unaweza kuvunja kizuizi hicho cha sauti kama... Wananiambia, wakati ndege inapojaribu kuvuka kizuizi cha sauti, karibu inang'oa makomeo yake, lakini baada ya kuvuka kizuizi hicho cha sauti, ni sawa, basi inaweza tu kwenda kasi kwa urahisi. Kama tunaweza tu kuvuka kutuama huko kwa—kwa ushirikina na kadhalika, basi Roho Mtakatifu anaanza tu kushuka kote, na, kama upako, na kuwabariki tu watu. Lakini watu wengi sana wa siku hizi wamebembelezwa sana, wanapapaswapapaswa tu, vitu *duni*.

<sup>8</sup> Niliona ono wakati mmoja huko Tulsa, Oklahoma, ambako nilikuwa tu nikifanya mkutano katika jumba kubwa la mikutano. Ndipo—ndipo mtu mmoja, akiwa mhudumu mahali fulani, alikuwa ameitwa mkutanoni, ninaamini mhudumu wa Kibaptisti, na kuanza kumwambia kuhusu maisha yake. Ndipo mmoja wa wachungaji wadhamini wa mahali hapo akampigia simu mtu huyu, na kumwuliza, “Hiyo ilikuwa ni kweli? Uliwahi kumjua Ndugu Branham?” Bila kujua ya kwamba ningejua yote kuyahusu katika chumba changu cha hoteli. Mnaona?

<sup>9</sup> Lakini, na kwamba mimi, baada ya Bwana kunifunulia yale aliyokuwa amefanya, vema, ndipo nikaangalia, na kwa kuwa mmoja wa hao watu alikuwa ameshuka, na kusema, “Sasa, Ndugu Branham, wakati akiwa chini ya upako, ni mtumishi wa Bwana, bali theolojia yake si nzuri.” Kasema, “Yeye ni nabii wakati upako uko juu yake, lakini,” kasema, “wakati upako umemwacha,” kasema, “loo, theolojia yake si nzuri.”

<sup>10</sup> Mtu ambaye angetoa tamshi kama hilo hata hajui maana ya neno *nabii*. *Nabii* linamaanisha, “mfunuzi wa Kiungu wa Neno.” Mnaona? Na ishara hizi ni thibitisho ya kwamba hiyo ndiyo kweli. Mnaona? Na, lakini, hapo tu ndipo mnapokuja, hayo madhehebu yanawafungia mahali *fulani*, ni—ni vibaya sana. Halafu mtu huko chini akiongea namna hiyo, kisha akashuka moja kwa moja, chumba changu cha hotelini, nami nilikuwa nikimwambia yale aliyosema. Vema, unalipata tu hivyo.

<sup>11</sup> Bila shaka mnaweza kuona, watu wengi sasa, kamwe hawatajua vita mpaka tutakapofika Ng'ambo ya pili, ndipo itafunuliwa ni nini, gharama inayolipa. Ambapo, unaketi

mezani pamoja na watu, na hadharani pamoja na watu, na kuona mambo hayo, huku mtu fulani anakupigapiga mgongoni, aseme, “Ndugu Branham, hakika tunakuunga mkono,” na bila kujua, papo hapo, ya kwamba ninajua huo ni uongo, mnaona, maana ninamwangalia tu moja kwa moja, nikijua ni nini hasa. Mnaona? Na hilo bila shaka linalifanya gumu. Mimi. . .

12 Mnafikiri mambo haya ni rahisi sana, na kitanda cha maua ya anasa? Lakini sivyo, enyi marafiki, ni *mapambano*. Loo, jamani! Afadhali nisilijue, a—afadhali nisilijue hata kidogo. Ninataka tu kuhisi mahali ambapo hata silioni, ama chochote kile, kusudi tu niweze kuendelea mbele, mwajua. Na kama unajua ya kwamba huyo mwanamume anakwambia jambo fulani lisilo sahihi, basi unajua, yeye akisimama hapo, ama mwanamke, ama yeyote yule, akijaribu kulifanya lisikike halisi sana, na hata hivyo, papo hapo, unaangalia ono, hilo ni kosa kabisa yale wanayosema, ndipo unajua hilo, na hilo, hakika ni jambo gumu.

13 Lakini kila mmoja wetu ana kazi ya kufanya, kila mmoja wetu ana huduma, na upekee wake, na kadhalika, yote kwa jumla ni ya kumtukiza Mungu, yote yakifanya kazi pamoja kwa wema.

14 Sasa, Bwana awe pamoja nasi na atusaidie. Nilikuwa nikiwazia, nililisema siku chache zilizopita, ya kwamba nilifikiri ningeanza na wale wapanda farasi wanne wa Ufunuo, kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa amebariki sana kwenye mikutano hiyo nyumbani majuma machache yaliyopita, juu ya zile nne, ama, zile nyakati saba za mwisho za kanisa, wale wahudumu, ama, malaika wa nyakati hizo za kanisa, na jinsi alivyozibariki.

15 Lakini basi nikaanza kuwazia, afadhali labda nirudi nyuma kidogo na—na kwa namna fulani kuliimarisha kanisa, kwa sababu ya mambo fulani Roho Mtakatifu. . . Ninaweza tu kunena kwa uvuvio, hayo tu ndiyo nijuayo, ningojee tu Yeye aliseme, ama, anipe, nami niliseme, hilo tu ndilo nijualo.

16 Nami nilikuwa nikimwambia mchungaji wenu asubuhi ya leo chumbani, kwamba mara nyingi ninasema mambo ambayo karibu yaniue kuyasema, lakini mtu fulani alisema, “Utaidhuru huduma yako kwa kufanya hivyo.” Ninawezaje kusema ila yale Yeye asemayo niseme? Mtu asipowaambia, itakuwaje? Ni ninii ya aina gani. . . ? Mnaona nini, kumekuwa na kupuuzwa sana kwake sasa. Mnaona? Hivyo ndivyo kanisa lilivyo katika hali kama hiyo sasa, kuna kupuuzwa kupindukia kwake. Mtu fulani hana budi kupiga kelele dhidi ya mabaya, si kwamba unawapigia kelele hao watu, ni makosa ambayo watu wamezibiwa ndani, wakijaribu kujifananisha na mtu mwingine, ama kufanya *hivi*, ama kitu kama hicho, wala hawamwangalii Mungu. Mnaona?

<sup>17</sup> Haidhuru jinsi...Kama mtu alikuwa akiniangalia mimi kama mfano, kamwe usifanye hivyo, nina mambo mengi sana mabaya maishani mwangu. Wewe angalia yule Mfano halisi, Yesu Kristo, Yeye alikuwa ndiye Mfano. Msiangaliane, mwangalieni Yeye, mnaona, Yeye Ndiye wa kuangaliwa.

<sup>18</sup> Sasa, basi nikawazia ningerudi usiku wa leo, na kwa namna fulani kuliweka Kanisa mahali pake katika Maandiko kabla hatujaingia kwenye Fundisho hili halisi, gumu, lenye nguvu la Kitabu cha Ufunuo. Ambacho ni, Kitabu cha Ufunuo, neno la Kiyunani *apocalypse*, ambalo linamaanisha “kufunuliwa,” kuondoa pazia kutoka kwenye sanamu, kweli, ndiyo Kiyunani kinamaanisha kwa hilo, kuondoa pazia kwenye sanamu, na kuwaacha watu waone kile kilichotengenezwa. Na ni ufunuo wa Yesu Kristo katika makanisa Yake. Ni kikuu, kwa sababu kinaonyesha kile Yeye alichokwa katika kila wakati. Nawe unaweza kuliona katika nyakati zilizotangulia, ulikuwa mkamilifu kabisa, hasa, na ndivyo ulivyo katika wakati huu, mnaona, kile hasa Yeye alichokwa.

<sup>19</sup> Sasa, hebu tumwamini Yeye, hebu tumwamini Yeye kwa mioyo yetu yote. Na, mnaona, jambo ni kwamba, linatupita sisi halafu sisi, kisha limekwisha, nasi tunashangaa lilikoenda. Mnaona, halafu tunaangalia nyuma, na, kwenye saa ya kufa kwetu, na kuangalia nyuma, tunawazia, “Vema, kama ninge—ningeninii...” Mnaona, imeenda mbali kupita kiasi wakati huo, kama tu vile hilo limekuwa katika kila wakati namna hiyo, na Biblia inasema itakuwa hivyo katika wakati huu.

<sup>20</sup> Moja ya mambo ya kuhuzunisha sana niliyopata kuona katika Biblia, Biblia ikibashiri, lilikuwa ni wakati huu wa kanisa. Huu ndio wakati wa kanisa wa kutisha sana kuliko nyakati zote za kanisa. Kila wakati wa kanisa...Angalieni Ufunuo, katika Laodikia, wakati wa kanisa la Kipentekoste, kwamba Kristo alikuwa ameondolewa katika kanisa Lake Mwenyewe, amesimama nje, akibisha, akijaribu kurudi katika kanisa Lake Mwenyewe. [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.]

<sup>21</sup> Sasa, ilionekana kama wito kwa wenye dhambi, bali huo ni wakati wa kanisa, wakati wa Laodikia. Alikuwa amefukuzwa na madhehebu, na kadhalika, walimweka nje, nao walikuwa wamechukua mambo ya ulimwengu, Naye akasema, “Nasimama mlangoni, nabisha.” Wa kanisa Lake Mwenyewe! Hakuna wakati mwingine uliofanya hivyo, bali wakati huu, kwa hiyo mnaona mahali tunaposimama. Mtu yeyote mkweli, mzuri, wa kiroho anaweza kulishika hilo, na kulitwaa, na kuambatana nalo, mnaona, kwa sababu mnaona mahali lilipo.

<sup>22</sup> Wachache sana, sana wa wakati huu watachukuliwa, kama tujuavyo. Watu wengi wanatazamia kuongezeka kwa wingi, mmiminiko, na kadhalika, kumbukeni tu, liwekeni alama

katika Biblia zenu: Hamtakuona, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Mnaona? Hamtakuona. Nao unaninii, wakati wa kanisa unakwisha sasa, huu ndio wakati, uko karibu kwisha, naye Mungu analivuta Kanisa Lake.

<sup>23</sup> Naye alitabiri ya kwamba Laodikia, vuguvugu vya kutosha kutapikwa kutoka kinywani, na huo ndio wakati hasa tunaishi, kila kitu kiko sawa kabisa kwa ajili ya wakati wa mwisho, na kila kitu. Tunaona kanisa katika hali hiyo, limeanguka ghafla, ni vuguvugu, vya kutosha kuninii, “Vema, unaonekana mzuri sana, mzuri sana. Labda nitarudi mwishoni mwa juma, tena.” Mnaona, hilo hapo, huo ndio msimamo wa kanisa. Ni wakati huo ambapo Mungu humchagua mmoja *hapa*, na *pale*, na mmoja kondeni, na mmoja, kadhalika, kumchukua.

<sup>24</sup> Kwa hiyo tunapoona tunaukaribia wakati huo, hebu na tutulie juu ya Neno la Mungu. Tuingie kwenye Neno la Mungu, Roho wa Mungu katika Neno, na hebu tuwe mawe hai, yaliyojengwa katika nyumba ya Mungu aliye hai.

<sup>25</sup> Sasa, usiku wa leo, ninataka kusoma sehemu ya Maandiko inayopatikana katika Mwanzo mlango wa 22 na kifungu cha 14:

*Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire, kama watu wasemavyo...Katika mlima wa BWANA... itapatikana...na hata leo.*

<sup>26</sup> Sasa, *Yehova-yire* maana yake ni, “Bwana atajitolea Mwenyewe dhabihu.”

<sup>27</sup> Sasa angalieni, tunarudi katika Mwanzo kwa ajili ya somo dogo kwa yapata dakika thelathini, ama arobaini, ndipo kesho usiku tutauchukua tena, kisha Jumamosi usiku, tuujenge. Nami nawatakeni myaandike Maandiko, mkitaka, nami nina machache yaliyoandikwa hapa chini kwenye ukurasa mdogo, kwenye karatasi yangu, na, kama nikiyatumia, mahali yalipo. Nasi tunataka kusoma, na kuchukua tu ki—kitu kama somo la Biblia katika Neno.

<sup>28</sup> Sasa, hili, bila shaka, ambapo tunaliita hili, Mungu ana yale Majina saba ambatani, ya ukombozi, *Yehova-Yire*, “Bwana atajitolea dhabihu”; *Yehova-Rafa*, “Bwana aponyaye”; na “Bwana Bendera yetu”; “Bwana Ngao yetu,” na kadhalika. Yeye huonekana katika Majina Yake ambatani, ya ukombozi.

<sup>29</sup> Na hiyo ni...Wakati Malaika wa Bwana alipotokea kule Houston wakati ule, wakati mhudumu wa Kibaptisti alipokuwa akijadiliana na Ndugu Bosworth, alimwuliza tu swali hilo moja, akasema, “Daktari Best, nitakuuliza: Je, yale Majina ambatani ya Yehova yalitumika kwa Yesu, *ndiyo* au *la*? Nijibu tu, *ndiyo* au *la*.”

<sup>30</sup> Naye asingejibu, kwa sababu, mnaona, kama angesema *ndiyo*, basi, huwezi kutenganisha Majina Yake ambatani, kwa hiyo kama Yeye ni *Yehova-Yire*, Dhabihu ya Bwana iliyotolewa,

Yeye pia ni *Yehova-Rafa* aponyaye magonjwa yetu yote. Kwa hiyo, na kama Yeye si *Yehova-Rafa*, wala si *Yehova-Yire*, Mwokozi wetu. Kwa hiyo kama Yeye si Dhabihu iliyotolewa na Mungu. . . Kwa hiyo huwezi kuwatenganisha. Hilo lilitosha, hilo lilikuwa ni—ni Andiko moja tu lililohitajika kutatua.

<sup>31</sup> Sasa, sababu ya mimi kuchagua kurudi nyuma katika Mwanzo, ni kwa sababu neno *mwanzo* linamaanisha, “mwanzoni.” Na hakuna dini duniani leo, hakuna dini potovu duniani leo, hakuna kitu duniani leo ambacho hakiwezi kutangazwa kutoka katika Kitabu cha Mwanzo. Ndio mlango wa mbegu, unarudi kwenye mbegu.

<sup>32</sup> Sasa, kama ulitaka kuona kitu chochote ni nini, angalia mahali kilipotoka, kifuatilie hadi kwenye mbegu. Sasa, ninarudi nyuma kulifuatilia Kanisa, Kanisa la kweli, kabla hatujaanza kuingia katika Ufunuo, kama Bwana akitujalia, kuwafanya mwone Kanisa la kweli ni nini, mahali lilipoanzia.

<sup>33</sup> Sasa, tungeweza kuingia kabisa katika Kaini na Habili, kulikuwako hasa, mwanzoni, kulikuwako na Kaini, mtu wa kidini, kulikuwako na Habili, mtu wa kidini. Na Habili na Kaini, wote wawili wakiwa ni ndugu, walikuja na kila mmoja akajenga madhabahu upande wa mashariki wa malango ya Edeni, hapo wote wawili walimwabudu Mungu, wote wawili walitoa dhabihu, wote wawili walijenga makanisa, ama, madhabahu, na wote wawili wakaabudu.

<sup>34</sup> Kama kujenga kanisa, kutoa dhabihu, kutoa zaka zako, na kadhalika, na hata kumwabudu Mungu, hakuhesabiwi haki, mpaka, isipokuwa uje kwa njia iliyowekwa na Mungu kwa ajili yake. Kwa kuwa kama ilikuwa tu kwamba ulienda kanisani, kwa hiyo ulikuwa mfuasi, kwa hiyo ukalipa zaka na matoleo yako, na kujinyyima ili kulijenga kanisa lenu. . . Huo ni uaminifu, hilo ni sawa, hayo yote ni dini, lakini hata hivyo Mungu alikataa la Kaini, kila toleo alilotoa, naye Kaini alikuwa tu wa kidini kama Habili alivyokuwa.

<sup>35</sup> Kwa hiyo kama kuwa wa kidini, na—na kwenda kanisani, na kulilipia kanisa, na kutoa dhabihu, na—na kuleta zaka zenu, na kumwabudu Mungu, kama hayo ndiyo yote Mungu anayohitaji, Yeye alikuwa—Yeye alikuwa, amefanya jambo la kikatali kumhukumu mtu aliyetimiza matakwa Yake. Hiyo ni kweli. Lakini, mnaona, “Iko njia ione kanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti.” Mnaona? Sasa, kuna njia ambayo Mungu huja, na hiyo ndiyo njia pekee utakayopata kuingia mle, ni kuja kwa njia aliyokuwekea Mungu. Hiyo ni kweli.

<sup>36</sup> Nayo Biblia nzima imejengwa, kabisa, juu ya ufunuo; Kanisa liko juu ya ufunuo, ufunuo wa Neno. Sasa, kumbukeni, Habili alimtoleaje Mungu dhabihu iliyo bora kuliko ya Kaini? Ilifunuliwa kwake. Kuthibitisha hilo, katika Mathayo

Mtakatifu, ninaamini mlango wa 12, wa 16, Yesu alisema, “Watu hunena Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?”

Na baadhi yao walisema, “‘Wewe ni Musa,’ na wengine, hao ni, ‘Eliya,’ na wengine, ‘nabii,’” na kadhalika.

Akasema, “Lakini ninyi mwasema Nani?”

<sup>37</sup> Ndipo Petro akanena, upesi, na kusema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

<sup>38</sup> Akasema, “Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, wala malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

Sasa, sasa, Katoliki inasema Yeye alilijenga juu ya Petro, kwa sababu alikuwa jiwe dogo. Kama ndivyo ilivyo, alirudi nyuma siku chache baadaye. Mnaona?

Mnasema, “Alilijenga...” Waprotestanti wanasema alilijenga juu Yake Mwenyewe, “Yeye ndiye Mwamba,” hilo ni kosa, bado.

<sup>39</sup> Alilijenga juu ya ufunuo wa kiroho. “Kufunuliwa, mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amelifunua.” Hiyo ndiyo sababu Yeye alimpa Petro funguo za Ufalme, alikuwa na ufunuo ya kwamba Yeye alikuwa ni Nani. “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.” Hiyo ni kweli, ufunuo wa kiroho wa Bwana Yesu Kristo.

<sup>40</sup> Wakati Mungu amemjulisha kwako kama Mtu, kama Mwokozi wako, kama Mungu wako, kama Mkombozi wako, kama Mponyaji wako, kama Mfalme wako, huyo Ndiye nanii... jinsi ufunuo wa kiroho unavyokuja.

<sup>41</sup> Sasa, tunarudi nyuma kumshughulikia Ibrahimu usiku wa leo, kwa sababu yeye ndiye aliyepewa ahadi. Sasa, nilisoma kutoka Mwanzo mlango wa 22 na kifungu cha 14, lakini kwa kweli tutarudi kwenye Mwanzo 12 kuanza, kwa sababu Ibrahimu, mwanzo wa Ibrahimu, alikuwa ameshuka kutoka Babeli, kutoka Shinari, na kuishi mabondeni.

<sup>42</sup> Nasi tunajua kuhusu Babeli, jinsi ambavyo Nimrodi alikuwa wa kwanza kujaribu kujiundia dhehebu. Aliunda shirika kubwa la kidini na kuyafanya makanisa yote madogo kumtolea ushuru, kwa mji huu mkubwa wa Babeli, na kujenga mnara kule uliopaa juu mbinguni, na kadhalika. Alidhani yeye, kwa mawazo yake mwenyewe aliwazia ya kwamba angeweza kufanya jambo ambalo lingewaokoa watu.

<sup>43</sup> Lakini wewe, hakuna kitu unachoweza kufanya kujiokoa mwenyewe, hakuna jambo moja, inakubidi kutumainia kwa uchaji neema ya Mungu kufanya hivyo. Huwezi kujiokoa mwenyewe, sijali wewe ni wa kidini jinsi gani, na jinsi

unavyojaribu kuwa mwema, na kushika amri zote, na kila kitu, hilo halitafanya jambo moja, hakuna jambo moja unaloweza kufanya kustahili chochote. Wewe kwa urahisi umepotea tu, na ni hayo tu. Hakuna njia kwako, kufanya, inakubidi kukubali njia Yake aliyoiweka, hiyo ni Yesu Kristo. Wewe, na ni bure, haikubidi kufanya jambo moja ila ukubali tu kile ulichopewa, hakuna jambo unaloweza kufanya.

<sup>44</sup> Kama mimi, tai yangu ilikuwa imepinda, nami ningemwambia Ndugu Buntain, “Ndugu Buntain, nitakupa dola milioni moja.”

<sup>45</sup> Naye akasema, “Asante, Ndugu Branham, nitainyosha tai yako,” kiasi *hicho*. Sikumpa, alifanya jambo fulani. Mnaona? Aliinyosha tai yangu kwa dola milioni moja. Unaona, huwezi kufanya jambo moja. Hakuna . . .

Watu husema, “Nilimtafuta tu Mungu, na kumtafuta Mungu.”

La, umekosea, ndugu yangu, hakuna mtu anayefanya hivyo, si—si wewe unayemtafuta Mungu, ni Mungu anayekutafuta.

Unasema, “Niliomba, nilifunga, nilimtafuta Mungu.”

La, Mungu alikuwa akikutafuta, maana Yesu alisema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza.”

<sup>46</sup> Ungewezaje kumwambia nguruwe amekosea kwa kula chakula kichafu? Mnaona, yeye kwanza kabisa ni nguruwe, hiyo ndiyo asili yake. Hivyo ndivyo ulivyokuwa, mwenye dhambi, kwa hiyo u—umetengwa, umekatiliwa mbali na Mungu. Wewe . . .

<sup>47</sup> Ungewezaje kumwambia chui madoa yake hayakuwa sawa? Unaona? Angewezaje kuyalamba kujaribu kuyaosha? Anayafanya tu maangavu zaidi. Hivyo ndivyo unavyojaribu kufanya, kuchukua dini upate kujipamba mwenyewe ili kujifanya kiumbe bora zaidi. Huna budi kutambua ya kwamba umekufa, hufai hata kidogo, wewe ni mchafu, na Mungu Ndiye pekee anayeweza kukusaidia. Hiyo ni kweli. Unapofanya hivyo, basi unaukaribia Ufalme wa Mungu, unapojihesabu kuwa si kitu, na kumtegemea tu Yeye kwa uchaji na kumwacha Roho Mtakatifu akuongoze. Hiyo ni . . .

<sup>48</sup> Nafikiri Kanisa limehubiriwa hata kufa, jambo linalohitaji sasa ni kurudi kwenye mafundisho, na kuwaweka kwenye msingi, kusudi upate kujua jinsi ya kujijenga mwenyewe katika—katika Kristo. Nasi tumejenga makanisa yetu juu ya mihemuko, na juu ya mambo mbalimbali, bali hatuwezi kujenga juu ya kitu chochote ila Kristo, ufunuo wa Yesu Kristo, hilo ndilo jambo pekee tunaloweza kufanya. Katika Yeye umekamilika, bila Yeye, umepotea, hakuna njia ulimwenguni kwako kuokolewa.

49 Sasa, wakati Mungu alipomwita Ibrahimu, alikuwa tu ni mtu wa kawaida. Ninawatakeni mjue, ya kwamba si lazima uwe mtu yeyote maalum ili Mungu akuite. Mungu hukuita kwa uteuzi, naye Ibrahimu aliteuliwa.

50 Alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano kabla Mungu hajamwita. Naye alikuwa amemwoa dada yake wa kambo, Sara, nao walikuwa wameishi pamoja kwa miaka mingi, naye alikuwa tasa.

51 Sasa, yeye alishuka akaja pamoja na baba yake katika kundi lililojiondoa Babeli, akashuka kuja hapa kwa Wakaldayo katika mji wa Uru. Labda waliishi katika hema, kama walivyofanya siku hiyo, wengi wao, watu maskini. Naye, mlo wake labda ulikuwa ni kula maforsadi, na kadhalika, na kwenda kichakani na kuwinda mnyama, na—naye aliishi maisha matulivu sana, lakini siku moja Mungu akasema naye. Sasa, hiyo hapo tofauti: Mungu anapozungumza na mwanadamu. Huenda alikuwa wa kidini, huenda alikuwa . . .

52 Vema, kama mtu yeyote aliwahi kusoma *Babeli Mbili* cha Hislop, na kadhalika, na kuona historia ya kale ya jinsi walivyokuwa na mwanamke huko juu ambaye alikuwa ni kuhani, ama kitu fulani, nao walikuwa na mizizi kutoka kwenye miti, na miungu, na vitu vingine vyote ambavyo nanii, kama Yakobo alivyokuwa navyo miongoni mwake, kabila, wakati alipomwacha baba mkwe wake, kwa hiyo walikuwa na kila namna ya mawazo ya udadisi.

53 Lakini Mungu alimwita Ibrahimu kama mtu binafsi alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, na kufanya agano naye.

54 Sasa, ninawatakeni mwone, wakati Mungu alipofanya agano Lake la kwanza, agano la Adamu, agano la Kiadamu, ilikuwa, Yeye alifanya hivyo kati Yake na Adamu, ndipo mwanadamu akageuka moja kwa moja na kuvunja agano Lake. Na kila wakati mtu anapofanya agano na Mungu, yeye hulivunja.

55 Lakini agano hili halikufanywa kati ya Mungu na mwanadamu, Mungu alifanya agano hili kwa nafsi Yake. Kwa jumla ni neema, hakuna—hakuna sheria kwake hata kidogo, Yeye kamwe hakusema, “Kama utafanya jambo fulani,” alisema, “*Nimefanya. Nimekubariki. Nimekufanya* baba wa mataifa. *Nimefanya.*” Agano kwa jumla ni neema, hakuna sheria kwake hata kidogo. Ni nzuri sana! Jambo pekee ambalo Ibrahimu . . .

56 Si kwamba tu alilifanya na Ibrahimu, sasa sikilizeni, hakulifanya tu na Ibrahimu, bali Uzao wake baada yake, Ibrahimu na Uzao wake baada yake. Hilo agano lilifanywa bila masharti kwa Ibrahimu na Uzao wake.

Unasema, “Vema, hao wangekuwa ni Wayahudi?”

La, bwana, hayo ni mataifa, “Nilikufanya baba wa mataifa mengi.”

<sup>57</sup> Je, mliona jina lake lilikuwa ni A-b-r- . . . -h-a-m, Abram, A-b-r-a-m-u, Abram. Ndipo alipobadilisha jina lake, alimpa jina la I-b-r—I-b-r . . . h-i-m-u, *Ibrahimi*, akichukua Jina Lake Mwenyewe, *Elohimu*, mnaona, akimfanya baba. Yeye ni Elohimu, Naye alibadilisha na kuweka sehemu ya Jina Lake juu ya Ibrahimu, kwa sababu yeye, kupitia ile ahadi iliyokuwa ije kupitia kwa Uzao wake, baba wa mataifa, Ibrahimu. Akabadilisha jina lake, akaweka sehemu ya Jina Lake kwa lake, sasa, akimfanya baba wa mataifa.

<sup>58</sup> Sasa angalieni, kwa Ibrahimu na kwa Uzao wake baada yake, sasa, si kwa *wazao* wake, bali *Uzao* baada yake. Ibrahimu alikuwa na wana wengi, bali Yule aliyeahidiwa alikuwa kupitia Isaka, na kupitia Isaka akaja Kristo, Uzao wa Kifalme, Uzao halisi wa Ibrahimu.

Sasa angalieni, mnasema, “Vema, Ndugu Branham, basi sisi ni nani?”

<sup>59</sup> Kama tuko ndani ya Kristo, katika Wagalatia 3, kama tuko ndani ya Kristo basi sisi ni Uzao wa Ibrahimu, nasi tu warithi pamoja naye kwa ile ahadi. Unaingiaje ndani ya Kristo? Kama umekufa kwa nafsi yako, umezaliwa katika Kristo, wewe ni Uzao wa Ibrahimu na mrithi wa ile ahadi pamoja na Ibrahimu. Basi kama wewe ni Uzao wa Ibrahimu, unaweza tu kuwa unapokuwa na ile imani aliyokuwa nayo Ibrahimu.

<sup>60</sup> Loo, sasa tuna—tunajiandaa kwa ajili ya ibada halisi ya uponyaji. Mnaona? Tunapoweza kuwazia juu ya a—ahadi yetu, Mungu anaweza . . .

Unasema, “Uliombewa jana usiku?”

“Naam, nilikuwa mkutanoni, mtu fulani akaniwekea mikono.”

“U mzima?”

“La, nilikosa uponyaji wangu.”

<sup>61</sup> Wewe si Uzao wa Ibrahimu, Ibrahimu aliamini. Biblia ilisema hakusita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, bali alikuwa na nguvu, akimtukuza Mungu.

<sup>62</sup> Ibrahimu alipoambiwa atampata mtoto huyu kwa Sara, za kwanza, ninawazia siku chache za kwanza, ama, siku thelathini za kwanza, alisema, “Unajisikiaje, Mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Utampata kwa vyovyote vile.”

Wakajitayarisha, wakafanya maandalizi kwa ajili yake. Basi siku zikapita, zikaendelea, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea, Ibrahimu: “Unajisikiaje, Mpenzi?”

“Hakuna tofauti.”

“Tutampata kwa vyovyote vile.”

<sup>63</sup> Kadiri ilivyoonekana haiwezekani, Ibrahimu alimsifu Mungu, maana itakuwa ni mwujiza mkubwa zaidi, ilikuwa kama ungetukia huko nyuma alipokuwa na umri wa miaka sitini. Amina.

<sup>64</sup> Halafu tunasema, “Naam, mimi ni Uzao wa Ibrahimu, bali nilikosa uponyaji wangu.” Ibrahimu aliita chochote kinyume na Neno la Mungu uongo, alikataa kuangalia chochote ila kile Mungu alichokuwa amesema, hicho kilikuwa ndicho kweli. Haidhuru ulimwengu ulisema nini juu yake, yale mtu yeyote mwingine aliyosema, yeye alijua yale Mungu aliyosema, alishikilia yale Mungu aliyosema. Halafu tunasema sisi ni Uzao wa Ibrahimu. Loo, rehema!

<sup>65</sup> “Nilipitia kwenye mstari wa maombi wa Ndugu Roberts, nitapitia kwa wa Ndugu Allen atakapokuja, ndipo Ndugu Branham atakapokuja, na hao wengine, nitapitia mstarini, nione kama nitapata uponyaji wangu.” Uzao wa Ibrahimu ati! Rehema! Si ajabu Yeye alisema atalitapika kutoka kinywani mwake, lilimchefua tumboni mwake. Naam. Loo, jamani!

<sup>66</sup> Uzao wa Ibrahimu unachukua ahadi ya Mungu, na chochote kinyume chake ni uongo, unaendelea moja kwa moja. Sasa, hebu tuone kama sisi ni Uzao wa Ibrahimu ama sivyo. Ningeweza kukipasua kitu hicho kwa hilo kama ningetaka, sasa hivi. Naam, bwana. Sara alitiije, yeye mwenyewe? Kama mke wa Ibrahimu. Sasa, lakini Uzao wa Ibrahimu unaamini ile ahadi, wakati Mungu anaposema jambo lolote hilo latosha milele.

<sup>67</sup> Basi kumbukeni, sasa, jambo lingine tunaloona, ya kwamba Ibrahimu, wakati alipopewa ahadi hii, ama Uzao wake, jambo pekee walilopaswa kufanya kutimiza agano lao lilikuwa ni kukaa katika nchi ya ahadi. Maadamu Ibrahimu alikaa katika nchi ya ahadi, hilo agano lingetenda kazi. Sasa, hilo tu ndilo walilopaswa kufanya. Hivyo tu ndivyo Uzao wa Ibrahimu unavyopaswa kufanya, hivyo tu ndivyo wewe unavyopaswa kufanya.

<sup>68</sup> Kama umejazwa na Roho Mtakatifu basi wewe ni Uzao wa Ibrahimu. Basi kama una Uzao wa Ibrahimu, ambao ni Roho wa Mungu ndani yako, akikufanya uamini kama Ibrahimu, ukiita kila kitu kinyume na Neno la Mungu kana kwamba ni uongo, Neno la Mungu ni kweli, usisitasite katika ahadi yoyote endelea tu kuishikilia, hilo hapo. Kama wewe ni Uzao wa Ibrahimu, basi kila kitu kinyume Nalo ni cha uongo. Ni Neno na Neno pekee, hapo nasimama.

Kama Eddie Perronet alivyoandika:

Nyote zisifuni nguvu za Jina la Yesu!

Malaika na wasujudu;

Ileteni ile taji ya kifalme,

Na kumtawaza kuwa Bwana wa wote.

Juu ya Kristo, Mwamba imara, ninasimama;  
Sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao.

<sup>69</sup> Huo ni Uzao wa Ibrahimu, sio kusitasita. “Haidhuru hali ya mambo inaonekanaje, yale sayansi isemayo, yale mtu mwingine yeyote asemayo, ni Neno la Mungu nami ninalishikilia,” huo ni Uzao wa Ibrahimu.

<sup>70</sup> Sasa, mnaona mahali kanisa la Kipentekoste lilipo siku hizi? Dhaifu kama maji ya tawi. Hiyo ni kweli, wanainama tu, kana kwamba nzi wanaanguka kutoka kwao. Uamsho ukianza, “Vema, siwezi kukaa muda mrefu sana, mhubiri huyo anahubiri zaidi ya saa moja. Ninaweza je kukaa hivyo?” Loo, ewe mfano duni, ewe maskini, mtu mwenye mashaka! Ati unajiita Uzao wa Ibrahimu, wakati Ibrahimu alitamani sana kusikia Neno la Mungu, aliomba, na akashikilia mpaka akapata ahadi, hapo akakaa, hivyo ndivyo Uzao wake unavyofanya, pia.

<sup>71</sup> Sasa, Uzao wa Ibrahimu ulipoteza lini ushirika huu mkuu? Aliposhuka kwenda Misri, kamwe hakupoteza agano lake, alipoteza baraka zake. Na hilo ndilo, ninalojaribu kuwaelezea ninyi watu, usiku wa leo. Kanisa la Kipentekoste limepoteza baraka zake za awali, kuna kasoro fulani, tunajua hilo. Mtu yeyote aliyewahi kusoma historia ya Kanisa anajua ya kwamba Kanisa lina kasoro. Sasa, hamjapoteza agano lenu, bali mmepoteza baraka zenu, rudini kwenye nchi ya ahadi, rudini kwenye Neno, mrudieni Kristo.

Acheni kuangalia, mkisema, “Dhehebu letu ni kubwa kuliko lao. Wao ni maskini viota vya koho, nasi tuko katika kitu ambacho...”

<sup>72</sup> Acheni kufanya hivyo, mrudieni Bwana Yesu, rudini kwenye Kanisa halisi. Nyosheni mikono yenu kwa kila ndugu aliyeanguka, haya basi, rudini. Mungu hajaondoa agano Lake kwenu, bali baraka zenu zimekwisha, kwa sababu mmekuwa wa kilimwengu, mliuendea ulimwengu, na kuanza kubembana na ulimwengu, ndipo mko nje ya ahadi, lakini agano bado linashikilia. Jambo pekee mnalopaswa kufanya ni kurudi, na halafu...

<sup>73</sup> Basi wakati Mungu alipofanya agano hili na Ibrahimu, kumbukeni lilikuwa bila masharti. Naye Mungu alikuwa, si kwa sababu ulikuwa mtu mzuri, lakini kwa sababu, bila masharti, Yeye alikuwa na kwa neema Yake akakupa Roho Mtakatifu. Ulikuwa Mlutheri, Mpresbiteri, Mkatoliki, na kwa neema Yake alikuwa na kukupa Roho Wake. Na jambo pekee unalopaswa kufanya ni kudumu katika Kristo, kwa kuwa hapo ndipo wewe...katika nchi ya ahadi.

<sup>74</sup> Wote walio ndani ya Yesu wako salama, na maadamu uko katika Mnara huu wa kimbilio katika Kristo, basi uko salama na mambo ya ulimwengu. Lakini unapoanza kuangalia nje, na kubembana na ulimwengu, jambo la kwanza wajua

unaanza kumwondokea Kristo. Sasa, ungali una lile agano, bali umepoteza baraka zako.

<sup>75</sup> Wamepoteza Roho mkutanoni. Piano inaweza kucheza, ngoma zinaweza kupigwa, na wanawake wenye nguo zilizobana vya kutosha mpaka, kama ngozi juu ya soseji, wakikimbia juu na chini sakafuni namna hiyo, wakiruka juu chini, hebu muziki ukome, wanasimama, pia. Hereni, na kila namna ya vitu vya kupendeza vya ulimwengu, huonekana kama namna fulani ya mchawi, badala ya—badala ya mtakatifu.

<sup>76</sup> Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikizungumza na mtu fulani akinipeleka, kanisa kubwa, naye akasema, alikuwa... akasema, “Mke wangu atacheza piano.”

Nikasema, “Hilo lingekuwa zuri sana.” Akaingia, na jamani, maskini mama huyo, jinsi alivyokuwa amevalia, naye akaketi chini, nikasema, “Ati yeye ni mtakatifu?”

Kasema, “Naam.”

<sup>77</sup> Nikasema, “Anaonekana kama *mtakataka*, badala ya *mtakatifu*.” Nikasema...Na hiyo ni kweli. Loo, jamani! Vitu kama hivyo si vya Kanisa la Mungu aliye hai, hivyo si vya watoto wa Ibrahimu, hivyo ni vitu vya ulimwengu. “Ukiipenda dunia, mambo ya ulimwengu, basi kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako,” ilisema Biblia. Hiyo ni kweli.

<sup>78</sup> Achaneni na mambo ya ulimwengu, mrudieni Mungu, rudini kwenye mikutano ya maombi, rudini kwenye—kwenye kitu halisi. Jitahiri, katilia mbali mambo ya ulimwengu. Omba mpaka Mungu atakapokushushia baraka Zake, vitu hivyo vife kama misumari ya milango, kisha urudi ndani ya Kristo.

<sup>79</sup> Sasa, sasa, agano hilo liliwadumisha Israeli mpaka walipofanya kosa lao la mwisho. Kutoka 19, mamia ya miaka baadaye, wakati Mungu alipokuwa...Angalieni kile neema ilichokuwa imetoa, lile agano lisilo na masharti, si kwa misingi yoyote hata kidogo, bali ilitolewa tu kwa neema. Walipokuwa wakisafiri kwenda kwenye nchi ya ahadi, kama vile Mungu alivyokuwa ameahidi, huku nyuma, Ibrahimu, na uzao wake ungekaa katika nchi ya kigeni kwa muda wa miaka mia nne chini ya utumwa, lakini ungetoka.

<sup>80</sup> Angalia, tayari walikuwa wametoka chini ya utumwa, Mungu, kwa neema, alikuwa amewapa nabii, Nguzo ya Moto, mwana-kondoo wa kafara, uamsho mkubwa sana waliopata kuwa nao, nao walikuwa wamesimama ufukoni wakicheza dansi, wakipiga tari, na wakiwa na yubile halisi ya Kipentekoste, kila kitu, maadui zao wote waliuawa nyuma yao, na kila kitu, na, hata hivyo, walitaka jambo la kubishania. Walitaka kupewa sheria ili waweze kuwa na kitu cha kuchangia kwake. Hivyo ndivyo hasa Pentekoste imefanya, kikamilifu kabisa, maana hiyo ilikuwa ndiyo mfano, ilibidi iwe hivyo.

<sup>81</sup> Angalieni, miaka arobaini iliyopita wakati baba zenu walipokuwa wakipaza sauti, na mama zenu huko nje wakiwa na baraka halisi za Kipentekoste, Mungu akifanya ishara na miujiza na mambo makuu, jinsi . . . mbona, mlidhani ule Utawala wa Miaka Elfu ungeingia moja kwa moja, lakini mlifanya nini? Laiti mngeliachilia tu, mwache tu neema ya Mungu iwaongoze! Lakini mtu fulani aliinuka na ile Hoja Mpya, kwa hiyo kundi *hili* likajiondoa, “Hatuamini upuuzi huo.”

Hili lingine, “Hatuamini upuuzi huo.”

Ndipo mmoja akasema, “Anakuja amepanda farasi mweupe.”

Huyo mwingine akasema, “Anakuja juu ya wingu jeupe.”

“Vema, jiundie dhehebu, umpandishe farasi mweupe, nami nitampandisha wingu jeupe.”

<sup>82</sup> Mnaona, lilifanya nini? Lililigawanya Kanisa, li—liliulaani ushirika wenyewe wa Mungu, iliwachukua watakatifu wa Mungu na kuwasambaratisha, na kuwatenganisha. Kisha mkafanya nini? Mkaketi papa hapa kwa miaka arobaini katika madhehebu yenu, mkiyanenepesha, na kufanya mambo makubwa mmo, basi mna nini sasa? Pia mmepata nini sasa? Endeleeni tu, na mbaki mumu humu nchini, mkitaka.

<sup>83</sup> Lakini ulikuja wakati ambapo Mungu alimwinua Yoshua, na kusema, “Hebu twende kwenye nchi ya ahadi. Hebu tuvuke.” Nafikiri hiyo ndiyo saa sasa, ambayo Mungu anajaribu kuwaleta watu wachache, “Na tuziendee ahadi kamili za Mungu.”

<sup>84</sup> Mungu alipowajalia kunena kwa lugha, mlisimama juu ya hilo. Msisimame hapo, hilo ni jambo moja tu, jamani, kuna, ya—yale maghala makuu ya Mungu yamejaa baraka nyingi za kila kitu, ahadi zote. Lakini ilitubidi kukoma, “Naam, sisi ni Wapentekoste.”

Vema, walileta hoja, wakaanza kubatiza katika Jina la Yesu, huyo mwingine akasema, “Kuna Miungu wawili.”

Mmoja akasema, “Wako watatu.”

Mmoja anasema, “Yupo mmoja.”

Mmoja anase- . . . Loo, jamani! Ndipo wao . . .

<sup>85</sup> Kwa nini msiachane nayo? Kama si la Mungu, hivi Yesu hakusema, “Kila mmea asioupanda Baba Yangu utang’olewa.” Achaneni nalo tu, udumisheni ushirika wenu ukiendelea, kwa vyovyote vile, kama si wa Mungu, utabatilika, kwa vyovyote vile. Usivunje ushirika wetu, na kujileta wenyewe *hapa* juu ya maskini mti wetu wenyewe. Hebu na tutupe tu mikono yetu na tumpende ndugu huyo, kama amekosea hebu tumwombe, tumrudishe kwenye ushirika tena, tuachane naye.

<sup>86</sup> Lakini la, ilitubidi tu kuendea jambo lile lile ambalo Kutoka kililiendea katika mlango wa 19. Walitaka sheria ili waweze

kujifanyia madaktari wa uungu na kuwa na theolojia yao, baada ya neema kuwapa kila kitu walichokuwa nacho. Mnaona? Wakati wasio wa kimadhehebu walipokuwa wamewaletea watu baraka za Kipentekoste, lakini basi iliwabidi kwenda na kuunda madhehebu kutoka kwake. Mnaona? Ni jambo lile lile tu lililofanya wakati huo. Ndipo mkaketi miaka arobaini, wala hakuna lingine.

<sup>87</sup> Walifanya nini? Hivi umewahi kuwazia yale waliyofanya katika miaka hiyo? Loo, Mungu aliwabariki. Walikuza familia, na mazao mazuri, na kuwafanikisha, hakika waliwafanikisha, na kila kitu, lakini hata hivyo walipungukiwa na baraka, hawakuwa katika nchi ya ahadi, bado. Sasa, lakini siku moja walienda kwenye nchi ya ahadi, kizazi kipya kikatokea, ndipo Mungu akawatuma katika nchi ya ahadi.

<sup>88</sup> Sasa, ujumbe wa neema ya Mungu, lile agano lisilo na masharti, lilikuwepo tangu wakati ambapo Mungu alimpa Ibrahim (Tutalifikia moja kwa moja, na kuonyesha jinsi Yeye alivyolithibitisha kwake.), ndipo basi hilo lilidumu hadi Kutoka, na ndipo walipofanyika washika sheria, na watoa sheria, na kadhalika, ambapo, wajilichukulia jukumu ili waweze kuwa na kitu cha kufanya ndani yake, ili waweze kuwa na jambo la kufanya. Kama tu vile Nimrodi, ilimbidi awe na jambo la kufanya, kwa hiyo akajijengea mnara, bali Mungu alimwonyesha tu Yakobo ngazi, neema.

<sup>89</sup> Lakini hivyo ndivyo imekuwa, hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, hatuna budi kufanya jambo fulani. Baadhi ya makanisa husema, “Sasa ngoja, unajua Dk. *Nanii* ndiye mchungaji wetu. Dk. *Nanii*. Sasa, hatuna mmoja wa maskini wahubiri hawa duni wa mbili kwa nne kule chini,” maskini Matendo 2 na 4, mwajua, “tunaye Dk. *Nanii*, Ph.D., LL.D. Yeye ni—yeye ni mhitimu wa Hartford,” ama kitu kama hicho.

<sup>90</sup> Mbona, afadhali mtoto wangu awe pamoja na mtu ambaye asingetofautisha maharagwe yaliyopasuliwa na kahawa, bali nijue ya kwamba amejazwa na Roho Mtakatifu, kuliko mtu mwenye digrii za kila namna ambaye hajui zaidi juu ya Mungu kuliko vile Mhotentoti angejua kuhusu hekaya za Kimisri. Naam, bwana. Tunachohitaji leo hii ni kurudi kwenye Ujumbe halisi, kurudi kwenye ninii, moja kwa moja kurudi kwenye wokovu dhahiri kabisa wa Pentekoste, chini, wa kale, wa moyoni, uliotumwa na Mungu, kuurudia Ujumbe.

<sup>91</sup> Tunapatana kupita kiasi siku hizi, kuachilia. Wahudumu wenye mipango mikubwa ambayo wanasema, “Siwezi kuwaambia watu hilo kwa kuwa hawangenidhamini.” Mbona, Mungu ndiye Mdhamini wetu. Mbona, jamani, wewe sema ukweli, kisha uangalie yale Mungu atakayokufanyia. Lakini mnaona, tuna mengi sana ya hayo nchini siku hizi.

<sup>92</sup> Sasa, tunaona baada ya kipindi hiki cha wakati basi, kiliendelea, kipindi hicho cha wakati huo wa kisheria, mpaka yule Uzao halisi wa Kifalme alipokuja, ndipo akajitwika ushika sheria wote juu yake Mwenyewe, na kulipa gharama ya ukombozi, ndipo Kanisa la Mungu limerudi katika neema tena. Si chini ya torati na sheria, liko chini ya neema na ahadi ya Mungu, Uzao wa kweli wa Ibrahimu. Alijitwika sheria nayo sheria ikamtundika msalabani, juu ya yale hatuna budi kufanya, na ambayo hatupaswi kufanya, na yanayotubidi kufanya, na ambayo hatupaswi kufanya.

<sup>93</sup> Mnajua mambo yake siku hizi, wakati mwenye dhambi anapomjia Bwana, ha—hatuwatendei kama Paulo alivyofanya wakati yule mlinzi wa gereza la Filipi aliposema, “Nifanye nini nipate kuokolewa?”

Sasa, tungenesema nini leo? “Huna budi kuacha kuvuta sigara, huna budi kuacha kunywa pombe, huna budi kuacha kufanya *hivi*.”

Hilo silo alilouliza, alisema, “Nifanye nini nipate kuokolewa?”

Ndipo Paulo akamwambia, “Mwamini Bwana Yesu Kristo.”

<sup>94</sup> “Mwamini Bwana Yesu Kristo.” Sio, “Njoo, ujiunge na kusanyiko letu, usimame mbele ya kanisa, na useme *hivi*, nasi tutakunyunyizia, tutakutumbukiza, ama chochote unachotaka kufanya, njia *yetu*. Na kama huko kanisani *mwetu*, basi...” Halikuwa hilo.

Alisema, “Mwamini tu Bwana Yesu Kristo, nawe pamoja na nyumba yako mtaokolewa.”

<sup>95</sup> Kama unaweza kuamini kwa ajili yako mwenyewe, unaweza kuamini kwa ajili ya nyumba yako, pia. Kuwa na imani ya kutosha katika Mungu kuamini kwa ajili yako mwenyewe, kisha uamini kwa ajili ya watoto wako, pia. Kuwa na... Imani iyo hiyo itawaokoa watoto wako iliyokuokoa, kama ukiendelea tu kuomba. Mungu atajibu maombi, usiwe na wasiwasi. Mwombe tu, na uamini, na ulitie nanga moyoni mwako, endelea tu kusonga mbele, hivyo ndivyo inavyofanywa. Naam, bwana.

<sup>96</sup> Sasa, tunaona ya kwamba Ibrahimu alikuwa tu ni mtu wa kawaida, naye Mungu akamwita, na kusema ya kwamba kupitia kwake atamfanya baba wa mataifa, “Haidhuru unafanya nini, Ibrahimu, haikubidi kufanya jambo moja, nimelitenda.” Loo, napenda hilo! Loo, ninapenda hilo sana, hata mimi... Linasisimua tu moyo wangu kuwazia si kitu ningeweza kufanya. Kama kulikuwa na jambo lolote ningaliweza kufanya, kamwe nisingelilipata, bali ni kile Yeye alichonifanyia. Si kile nilicho mimi, kile alichu Yeye; si kile ahadi yangu ilicho, ni kile ahadi Yake ilicho.

<sup>97</sup> Hivyo ndivyo watu siku hizi, inawabidi kuwa na... Sasa, wengi wa ndugu wanaoweka mikono juu ya wagonjwa, hilo ni sawa, lakini hayo ni mapokeo ya Kiyahudi, ambayo kamwe hayakukusudiwa kwa ajili ya Mataifa.

Myahudi alisema, “Njoo, uweke mkono Wako juu ya binti yangu, naye atakuwa mzima.”

Lakini Mmataifa alisema, “Sema tu Neno, mtumishi wangu ataishi.” Hiyo ndiyo tofauti. “Sema tu Neno.”

Yesu aliwageukia Wayahudi, akasema, “Sioni imani kama hiyo katika Israeli.”

<sup>98</sup> Mnaona, katika mikutano, kila mtu anayekuja mikutanoni anapaswa kumwamini Bwana Yesu Kristo. Kama... Yesu tayari amekuponya, “*Alijeruhiwa* kwa makosa yako, kwa kupigwa Kwake wewe *uliponywa*,” tayari, wakati uliopita, tayari imekwisha. Unaninii tu... “Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno.”

<sup>99</sup> Unasema, “Vipi kuhusu huo upambanuzi na mambo uliyokuwa ukifanya, Ndugu Branham?” Hilo ni thibitisho, hilo linathibitisha ya kwamba Yeye hutimiza Neno Lake. Yeye aliahidi ya kwamba angefanya mambo hayo, Huyu hapa akiyafanya. Kama akitimiza Neno moja, Yeye hutimiza Neno Lake lote. Asipotimiza Neno moja, hatimizi lolote la Hilo; Yeye hutimiza Neno Lake lote.

<sup>100</sup> Hawezi kukuponya, kama alikuwa akitembea papa hapa sasa, papa hapa katika jengo hili, asingeweza kukuponya, kama ungeweza kumwona akionekana, kama vile ungeniona mimi, ama mchungaji, ama mtu mwingine, asingeweza kukuponya, tayari amekuponya. Lakini huenda akakuonyesha sababu fulani, kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Bwana wako, maana angefanya kitu kama alivyofanya huko nyuma kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Bwana wako.

<sup>101</sup> Sasa angalieni, tunaona ya kwamba Ibrahimu, Mungu alimwambia, akasema, “Sasa, jitenge na jamaa zako, jitenge na jamaa zako wote, toka, uwe pamoja Nami nami nitakubariki.” Loo, hilo si ni zuri sana? “Nitakubariki kama utajitenga.” Lakini hapo ndipo shida inapokujia.

<sup>102</sup> Hapo ndipo shida inapojia, watu hawataki kujitenga, hawataki kujitenga na karamu zao za karata, mambo ya ulimwengu, unajaribu kuleta hilo moja kwa moja kanisani pamoja nao. Inakubidi kujitenga na wasioamini, usijifunge nira pamoja na wasioamini, “Tokeni, mkajitenge,” asema Bwana.

<sup>103</sup> Sasa, ulimwengu unatafuta wachanganyaji. Mnajua, mara nyingi, nilipokuwa katika kanisa lingine la kimadhehebu, walizoea kuniambia, kusema, “Sasa,” wangesema, “Wao—wao... Yeye ni mchanganyaji mzuri sana. Ninaamini kwamba tungemtuma *huko* chini... Hakika, anawachukua wanawake

wote na waume zao na kwenda kuogelea, yeye—yeye hucheza karata pamoja nao, kisha wanacheza dansi huko chini kwenye orofa ya chini, na loo, ni mchanganyaji mzuri.”

<sup>104</sup> Mungu hataki wachanganyaji, anataka watenganishaji, “Nitengeeni Paulo na Barnaba.”

<sup>105</sup> Mungu anataka watenganishaji, ulimwengu unataka wachanganyaji, maskini Hollywood, nywele pindokombo, na kadhalika namna hiyo, anayeweza kusimama, na kuchanganyikana na umati. Nao wa—watu wanataka ujana, wanataka maskini jamaa mdogo ambaye ndiyo kwanza atoke chuoni, anayejua vidokezi vyote, na kadhalika.

<sup>106</sup> Watamchukua jamaa mdogo kama huyo, lakini hebu iwabidi kufanyiwa upasuaji wakati mmoja, uone kama watamchukua daktari mpya ambaye ndio kwanza atoke, huo ndio upasuaji wake wa kwanza. Loo, la, kwa kupasua hiyo anatomia unataka maskini daktari mpasuaji anayejua yale aliyofanya, ambaye amekuwapo. Hiyo ni kweli. Bila shaka unaujali sana mwili huu, lakini vipi kuhusu nafsi yako, ukiwaruhusu baadhi yao kuipasua hiyo?

<sup>107</sup> Mwili wako utakufa, utaangamia, hiyo ni kweli, bali una nafsi iliyo ya Milele, lakini hutaki kumchukua mtu ambaye amekuwa katika huduma kwa muda mrefu, na amepitia vitani, na kupata ujuzi, na kusimama karibu na wafu, na wanaokufa, hasa, na kuwaangalia walipokuwa wakifa, na kuona ninii. . .

<sup>108</sup> Maskini matukio hayo hayafai kitu, yatatoweka kama kila kitu wakati mauti yanapomgusa mtu, daktari anawadunga sindano ya kuwachangamsha, na kuwasikia wakilia wapate rehema, na kupaza sauti, na kila kitu, hilo halifai kitu (Lakini nawaambia, maskini kisa kizuri cha wokovu, anamtazama Yesu Kristo usoni kwa moyo safi, na kumsifu Mungu, anakufa ukinena kwa lugha, naam, bwana, mtakatifu halisi wa Mungu, huyo ndiye anayeshikilia siku hiyo, kwenye saa ya mauti. Mnaona?), na huyo ni jamaa fulani anayejua theolojia nyingi sana, wala hajui chochote kumhusu Mungu; hatuna budi kujua Mungu ni nini, kumjua Yeye kwa tukio la kibinafsi.

<sup>109</sup> Sasa, Yeye alisema, “Jitenge,” lakini je, Ibrahimu alifanya hivyo? La, bwana. Na Mungu kamwe hakumbariki mpaka alipotii kikamilifu yale Mungu aliyosema afanye. Sasa, nitaliambia Kanisa hivi: Kanisa halitaendelea mbele zaidi, mpaka mtakapotii kikamilifu yale Mungu aliyosema mfanye, kamwe hamwezi kuendelea mbele. Mungu anatoa ahadi, Ibrahimu alizunguka-zunguka, na kadhalika, na Mungu kamwe hakumbariki kikamilifu mpaka tutakapoingia katika mlango wa 13 wa Kut-. . . wa Mwanzo.

<sup>110</sup> Nasi tunaona basi kwamba kulitokea ubishi mdogo kati ya wachungaji, na kadhalika, naye Mungu aliona hilo likija, kwa hiyo Ibrahimu, akiwa kama Mkristo, alimwambia mpwake Lutu,

akasema, “Kusiwe na ugomvi kati yetu, kwa kuwa sisi ni ndugu.” Akasema, “Sasa, wewe jichagulie, kama ukienda upande wa mashariki, nitaenda magharibi; na ukienda magharibi, nitaenda mashariki. Chukua tu...” Huyu ni mwungwana Mkristo halisi. Mnaona? “Ninyi nendeni njia moja, nami nitaendea hiyo nyingine. Hebu tusibishane, hebu wachungaji wetu wasibishane.”

<sup>111</sup> Vema, Lutu, akiwa mlafi, alionyesha kile alichokuwa, aliangalia chini kule akaona vitu vikuu tayari vimejengwa, hakutaka kutembea na Mungu peke yake, alitaka kuchanganyikana na ulimwengu.

<sup>112</sup> Hivyo ndivyo kanisa lilivyofanya hasa. Badala ya kutembea na Mungu, ililibidi kujiondoa na kujichanganyisha na ulimwengu. Mnaona mahali tulipo usiku wa leo? Mnaona mahali kanisa lilipo? Hiyo ni kweli kabisa, rafiki.

<sup>113</sup> Lutu alikuwa kule chini, mlafi, naye akashuka Sodoma, ndipo akaendelea kujongeza hema lake huko, maana labda Bibi Lutu alitaka nguo kama zile walizokuwa wakivaa huko Sodoma, naye alitaka kuwa hivyo, naye Lutu alitaka kuwa mfanyabiashara mashuhuri, mwenye ushawishi mjini, kwa sababu alidhani labda angeweza kupata dola chache za ziada, ama kitu fulani. Ndipo basi yeye, akaona, alikuwa na wadhifa mzuri kule chini, bali alikuwa amerudi nyuma, alikuwa amerudi nyuma. Sasa, hilo ni kanisa la kimwili.

<sup>114</sup> Akashuka akaenda Sodoma, naye akashuka kule na kuchanganyikana na walimwengu, walikokuwa wapotovu na kadhalika, ndipo akawapeleka binti zake kule chini, kisha akawachukua nanii wake, watoto wake wote, mke wake na kila kitu, na kuwaweka moja kwa moja katika mchanganyiko wa kundi kama hilo.

<sup>115</sup> Basi wakati alipojitenga, kwa sababu hilo lilikuwa ndani yake hapo mwanzo, basi wakati alipojitenga kabisa, ndipo Mungu akambariki Ibrahimu, akasema, “Ibrahimu, ulichukua njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Ulijitenga ukae hapa nje kwenye nchi kame, na sasa nitakubariki, kwa sababu nitakupa kila sehemu ya nchi hii, kwako wewe na uzao wako baada yako, nitakupa yote.” Sasa, Yeye alisema, “Simama tu na uangalie mashariki, kaskazini, magharibi, na kusini, na utembe kote nchini.” Amina. Ninapenda hilo. “Tembea kote, yote ni mali yako.”

<sup>116</sup> Loo, napenda hilo. Ni kama tu njia tao kubwa ambayo tumebatiziwa, kwa kuwa kwa Roho mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja. Na katika Mwili huo ni Kristo Yesu, na kwa Roho mmoja tumebatizwa kuwa Mwili huo, na kuwa washiriki wa Mwili huo. Haya basi.

<sup>117</sup> Mnaona, sasa, kama vile ninii...Ni njia tao kubwa. Sasa, watu wengi ndio kwanza waingie, wanasema, “Vema,

nitamkubali Yesu kama Mwokozi wangu, wala sitaki anipeleke kuzimuni, bali ni—nitamkubali kama Mwokozi wangu, nitasimama papa *hapa* ndani.” Lakini hivyo sivyo ilivyo, kama una uwanja mkubwa wa njia tao, zunguka, uone kile ulicho nacho.

<sup>118</sup> Sasa kwenu ninyi Wabaptisti, Wamethodisti, na Wapresbiteri, kama hamwamini Roho Mtakatifu ni wa kweli, kama hamwamini uponyaji wa Kiungu ni wa kweli, kwa nini msichunguze kwenye Njia Tao? Angalieni kote, vuteni mtoto huyu wa meza. Kama mtu akinipa nyumba kubwa, ningezunguka-zunguka, nione mali yangu, mimi ni mdadisi, ninapenda kuzunguka, nione yaliyo yangu.

<sup>119</sup> Vema, nilipomjia Kristo, nilitaka kuona nilichokuwa nacho. Amina. Nikaona uponyaji wa Kiungu ulikuwa ni wangu, furaha ilikuwa ni yangu, mito ikitiririka, Uzima wa Milele, nguvu, Uzima wa Milele, neema, mambo haya yote yalikuwa ni mali yangu. Kitu fulani kilionekana kiko juu kidogo, nikajitafutia ngazi, na kupanda juu, na kujivuta juu, na kukiangalia. Hiyo ni kweli. Kama nikiona kitu ambacho siwezi kukifikia, ninaendelea tu kuombea kwenye ngazi ya Yakobo mpaka nitakapofika hapo juu na kukiangalia.

<sup>120</sup> “Naam, Bwana,” ninaona mahali anapotoa maono, “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya. Mambo nifanyayo, mtayafanya. Nitakuwa pamoja nanyi. Ombeni mtakalo, nitawapa.” Hayo yote ni yangu, mimi ni mrithi, amina, mrithi. Kupitia mauti ya Yesu Kristo, ninakuwa mrithi wa kila kitu, kila ahadi. Mimi ni mrithi, kwa hiyo nina haki ya kuangalia pande zote, nione kile *nilichorithi*.

<sup>121</sup> Vipi kama mtu fulani alisema ulikuwa na mtaa mkubwa hapa chini California mahali fulani ambao *ulirithi*, mtu fulani alikuachia wosia? Je, ungesema, “Loo, nadhani ni sawa”? Loo, la! Ungeondoka uende kule, ndugu, na ungechukua mawakili, na kadhalika, nawe ungeona mali uliyo nayo. Hutaninii... kuchukua kuhusu maisha haya, maisha haya—haya ya kawaida, bali inapofikia Uzima wa Milele, wakati umemkubali Yesu Kristo kama Mwokozi, mbona usiangalie urithi wako? Amina.

Kila ahadi katika kile Kitabu ni yangu,  
Kila mlango, kila aya, kila mstari. (Hiyo ni kweli.)

Ninatumainia upendo Wake wa Kiungu,  
Kwa maana kila ahadi katika kile Kitabu ni yangu.

Mimi ni mrithi wa vitu vyote katika Kristo, mimi ni mrithi wa uponyaji wangu, mimi ni mrithi wa furaha yangu.

Mimi ni mrithi wa wokovu, nimenunuliwa na Mungu,

Nikazaliwa kwa Roho Wake, nikaoshwa katika Damu Yake.

<sup>122</sup> Naam, bwana. Mimi ni mrithi, mtoto wa Mfalme, mimi ni mwana wa Mungu. Amina. Kila kitu ambacho Mungu aliahidi ni changu. Mimi ni warithi pamoja na Bwana Yesu. Amina. Ninapenda kuangalia kote.

Kasema, “Ibrahimu, toka nje ukaangalie kote nchini, uone mali yako. Unaona *kile*? Hivyo vyote ni vyako.”

<sup>123</sup> Loo, ninapenda hilo. Angalia pande zote, uone kile kinachokuja kwako. Kwa nini usiende kesho ukaangalie katika Biblia uone, wewe, uone wewe ni mrithi wa nini? Uangalie tu baraka hizi zote kuu ambazo—ambazo Yeye alikuahidi, wewe ni mrithi wake, ni zako, hukustahili chochote, bali *ulirithishwa* kupitia kwa Uzao mwenye haki wa Ibrahimu, ambao ulikuwa ni Yesu Kristo. “Sisi, tukiwa wafu katika Kristo, tunachukua Uzao wa Ibrahimu, nasi ni warithi pamoja Naye wa ile ahadi.”

<sup>124</sup> Basi kama wewe ni Uzao wa Ibrahimu unaamini kila kitu alichosema Mungu, Mungu alisema, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Mimi ni mrithi wa hilo. Amina. *Nilirithishwa* hilo. Vema, baraka hizi zote alizoahidi, mimi ni mrithi wake. Ndipo mimi—mimi ni . . . hiyo—hiyo ni mali yangu.

<sup>125</sup> Mungu anapomwokoia mwanadamu humpa kitabu kikubwa cha hundi. Hapo chini kina kila kitu . . . Jina la Yesu limeandikwa juu yake, chini ya hicho kitabu cha hundi. “Lolote utakaloomba katika Jina Langu, hilo nitalifanya.” Uzao wa Ibrahimu unaamini hilo. Jaza tu hiyo hundi na uitume, amana tayari imefanywa, iko kwenye benki.

<sup>126</sup> Ilipitiaje? Si kwa haki yako, bali kwa haki ya yule Uzao wa Kifalme mwenye haki, Kristo. Yeye Ndiye aliyeweka ile amana mle ndani, amana iko kwenye benki. Ninaamini hilo, sivyo? Basi usiogope kuandika hundi, benki itailipia, Benki ya Mbinguni italipia kila hundi. Naam, bwana.

<sup>127</sup> Jambo la kwanza, inabidi ipitie kwenye ofisi ya kubadilisha hundi, hiyo ni kweli, kuona kama kweli unaamini ama huamini. Kama unaamini, itapita kwenye chumba cha kubadilishia hundi, usiwe na wasiwasi kuhusu hilo, na hizo pesa zitakurudia mara tu itakapopitia kwenye chumba cha kubadilishia. Hiyo ni kweli.

<sup>128</sup> Kama ndani ya moyo wako unaamini kweli hiyo ni ahadi ya Mungu, nawe umeikubali moyoni mwako, ombeni katika Jina la Yesu Kristo, inarudi. Mungu aliahidi hivyo; huyo ni mrithi. Sisi ni warithi wa wokovu na warithi pamoja Naye, nasi ni warithi pamoja na Ibrahimu, kwa sababu sisi ni Uzao wa Ibrahimu.

<sup>129</sup> Sasa, kama umefanya mambo mabaya, kama umetoka kwenye barabara ya kale inayopitiwa na kuingia upande wa ulimwengu, hujapoteza agano lako, dada, ndugu, hujapoteza

agano, umepoteza tu ba—baraka za agano. Rudini, tokeni Misri, rudini huku juu katika nchi ya ahadi, mkaingie ambamo Mungu alisema ya kwamba mnapaswa kukaa, “Mkikaa ndani Yangu,” Yohana Mtakatifu 15, “na Maneno Yangu yakae ndani yenu, mnaweza kuomba mtakalo, nanyi mtapewa.” Lakini kaeni humo ndani. “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu. . .” Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Ni ahadi ya Mungu.

<sup>130</sup> “Mkikaa ndani Yangu,” hilo linamaanisha kukaa mle. Msiwe mkikimbia kule Misri na kukimbilia mambo ya ulimwengu. “Mkikaa ndani Yangu, Maneno Yangu yakae ndani yenu, mwaweza kuomba mtakalo, nanyi mtatendewa.” Hiyo ni ahadi Yake. Kama wewe ni Uzao wa Ibrahimu, basi dumu katika ahadi hiyo. Kama uko nje yake, rudi kwake, utapata shida huko chini Misri, rudi kwenye nchi ya ahadi.

<sup>131</sup> Sasa, tunaona basi yeye alijitenga; naye Mungu kamwe hakumbariki Ibrahimu kabisa mpaka alipomtii kikamilifu na kujitenga. Wala Mungu kamwe hatambariki mtu binafsi, ama kanisa, ama kusanyiko, ama dhehebu, mpaka litakapojisalimisha kikamilifu katika kumtii Mungu.

<sup>132</sup> Madhehebu ni sawa kama mngaliliandika hivi: “Tunaamini katika hili, *koma*.” Lakini mnapoandika dhehebu, “Tunaamini jambo hili, *kituo kikuu*. Uje kwenye *hili* la sivyo usije kabisa.” Ukilisoma, “Ninaamini hili, *koma*, pamoja na yale Mungu atakayonionyesha,” basi ni sawa. Hiyo ni kweli. “Kama nitaninii. . . Ninaamini. . . Tuna. . . Tunaamini *hili*, pamoja na chochote tunachoweza kupata kutoka kwa Mungu kilicho bora zaidi.” Mnaona, lakini mnamalizia, “Tunaamini *hili*.”

<sup>133</sup> Ilikuwaje kwa Luther mara Luther alipoiona ile Nguzo ya Moto? Mbona, aliifuata. Lakini alifanya nini? Baada ya siku za Luther, waliunda kanisa lililoitwa Luther, ndipo likafa papo hapo kwenye madhehebu, maana ni kama tu kanisa Katoliki.

<sup>134</sup> Ndipo, muda si muda mwajua, akaja Wesley. Ile Nguzo ya Moto ikatoka moja kwa moja kwenye madhehebu, ikaendelea, Wesley akaiona, naye huyo akaifuatilia. Na mara duru ya zamu ya kwanza ilipokwisha, wakaliundia dhehebu, wakaliita Methodisti ya Wesley, ama ka—kanisa la Methodisti, walipoliundia dhehebu, lilikufa papo hapo.

<sup>135</sup> Ndipo Wapentekoste wakaiona ikitoka, si kutoka kwenye kuhesabiwa haki chini ya Luther, kutakaswa chini ya Wesley, bali waliona ubatizo wa Roho Mtakatifu, kurudi kwenye baraka asili. Hawa hapa wakamfuata, loo, jamani, wakatoka wakaanza kunena kwa lugha, na nguvu za Mungu zikitenda kazi kupitia kwao. Lakini walifanya nini? Wakaliundia dhehebu, likafa papo hapo. Lakini sasa Nguzo ya Moto inaondoka, inasonga tena. Kamwe haitaninii. . .

<sup>136</sup> Hakuna hata wakati mmoja ambapo dhehebu liliwahi kuinuka ambalo halikufa wala halikurudi tena. Ninampa changamoto mwanahistoria yeyote. Ninamtazama usoni pale mmoja wa walio bora sana katika taifa hili. Hiyo ni kweli. Mwanahistoria wa wanahistoria ameketi moja kwa moja pamoja nasi. Nami nitamwomba mtu huyo, ama mtu mwingine yeyote, kunionyesha wakati mmoja ambapo kanisa lilipata kujiundia dhehebu, bali halikufa na kubaki mfu. Kamwe halikuinuka tena katika historia ya makanisa ya ulimwengu, kamwe halikuinuka. Mungu hataki jambo hilo, Mungu anatutaka tuwe huru ndani Yake. Anatutaka tufikie mahali ambapo tunaweza kumkubali Mungu wote, sio kukaa kwenye mlima huu, tutoke nje; Uzao wa Ibrahimu.

<sup>137</sup> Sasa, mnasema, “Hivi unapinga dhehebu?” La, bwana. Madhehebu ni sawa, bali mnaweka mpaka, mnamkatilia mbali kila mtu ila yule jamaa asiyeamini kama tu mnavyoamini. Jambo tunalopaswa kufanya ni kuwanyoshea mikono yetu Walutheri, Wamethodisti, na wote, kufikia mahali ambapo tunaweza kuwa na ushirika sisi kwa sisi, huku Damu ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ikisafisha na dhambi zote, mpaka tutakapofika hapo, tutakufa tu, tuketi papa hapa na kusinyaa kama tofaa la kale lililonyauka.

<sup>138</sup> Na hapo unakuwa wa kukunjisha mdomo kama zaituni, na kuketi huku, “Vema, mimi ni *Fulani-wa-fulani*.” Loo, jamani! Hakuna Uhai tena unaoingia mle, mnaona (Kamwe hatuwezi kufanya hivyo. La, hatuna budi kuja na kuwa katika Kristo Yesu, sisi ni warithi, warithi pamoja Naye.), sasa, mpaka tutakapojitenga na mambo ya ulimwengu.

<sup>139</sup> Sasa, mnaona, kila kanisa linaanza kujifanya... Sasa, mnasema, “Hivi unanena tu juu ya Wamethodisti?” La, ninazungumza juu ya wote, kila mmoja wao, Pentekoste yetu, sawa tu na wao. Wala hakuna mtu mwenye moyo mwaminifu katika jengo hili ila yule anayejua kwamba kanisa la Kipentekoste linakuwa kama tu makanisa mengine. Ni wangapi wanaoamini hilo? Inua mkono wako. Asanteni kwa mioyo miaminifu. Hiyo ni kweli. Ni kama tu hao wengine, vema basi, hilo ni kosa, hilo si sahihi. La, bwana. Mungu hawezi kuundiwa dhehebu. Kile anachopaswa kuwa, ni kuaminiwa. Haleluya!

<sup>140</sup> Loo, ndugu, jinsi ambavyo Mungu atainua mambo ya kila namna kama Kanisa litakuwa tu katika hali ya kuyapokea, bali kamwe hatajenga msingi Wake juu ya kitu ambacho mwanadamu ameweka. “Kwa maana hakuna msingi mwingine uwezao kuwekwa, ila ule uliokwisha kuwekwa, Kristo Yesu, Mwana wa Mungu,” na ufunuo atakaojenga Kanisa Lake juu yake, wa Kristo Yesu. Naam, bwana. Kumfanya yeye yule jana, leo, na hata milele, Yeye ni Uzao wa Ibrahimu leo, kama alivyokuwa wakati huo. Nasi ndani Yake, sisi ni warithi pamoja

Naye, pamoja na baba Ibrahimu, kwa kuwa Yeye ni Uzao wa Ibrahimu, Kristo alikuwa ni Uzao wa Ibrahimu.

<sup>141</sup> Sasa, utengano kamili, hatuna budi kutoka nje. Unasema, “Ati nitoke kwenye dhehebu langu?”

La, kaa katika dhehebu lako, bali acha ulimwengu ukuondokee, ndivyo ilivyo, si dhehebu lako.

Unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa Assemblies.”

Hilo ni sawa na lolote la hayo.

“Mimi ni mfuasi wa Presbiteri.”

Hilo ni sawa na lolote la hayo.

“Mimi ni mfuasi wa Umoja, Uwili,” ama chochote kile.

<sup>142</sup> Hilo ni sawa na lolote la hayo, yote ni taasisi za kujibunia. Vema. Lakini hilo silo jambo. Je, wewe ni wa Kristo? Wewe ni Uzao Wake? Je, umekufa katika Kristo na ni Uzao wa Ibrahimu? Basi una imani katika Mungu aliye hai. Utakuwa mfano kwa hao watu wengine walio humo ndani. Simama, jifanye mwenyewe Mkristo halisi. Jitikise, mavumbi kutoka kwako, amka, jirudie, tuko vitani.

<sup>143</sup> Tuko katika Wakati wa Kanisa la Laodikia. Ni wangapi wangetambua tuko katika Wakati wa Kanisa la Laodikia? Loo, ndugu, hebu na tufanye jambo fulani kulihusu basi, hebu tufanye jambo fulani kulihusu. Hebu tusishikwe katika hali ya namna hiyo huku Kristo akiwa nje akijaribu kubisha apate kuingia, hebu na tumruhusu aingie. Tukiwa ndani Yake, basi sisi ni warithi wa kila kitu. Yote ni mali yetu. Loo, ninapenda hilo. Kila ahadi!

<sup>144</sup> Loo, siku chache baadaye usiku, baada ya kumalizia jambo hili, ninataka kumshusha kwenye Mlima wa Kugeuka Sura, nionyeshe yale Mungu aliyomfanyia pale, kuwekwa Mwanawe mahali pake, angalieni jinsi anavyowatoa wana wengine, na kufanya jambo lile lile. Loo, jamani, ni utajiri mkuu jinsi gani ulio katika Biblia hii! Acheni kusoma hadithi za kale za kuchekesha, na kuangalia maskini vipindi vibaya vya televisheni, mrudi kanisani, kuomba.

Na kwa hiyo, mnasema...mwanamke mmoja alisema, “Vema, si—siwezi kupata wakati wa kuwasomea watoto wangu Biblia yangu.”

<sup>145</sup> Mbona, Susanna Wesley, alikuwa na watoto kumi na saba, naye alitumia saa tatu kwa siku, bila vyombo vya kisasa, hakubonyeza kitufe, akaosha vyombo vyake, hakufungua bomba na kutoa maji kidogo namna hiyo, aliyabeba kutoka kwenye chemchemi katika ndoo kuukuu ya mbao na kibuyu, akayabeba kutoka kwenye chemchemi, na kuwalea watoto kumi na saba, na angeweza kutumia saa tatu kwa siku katika maombi. Aliwalea akina nani kutoka kwake? John na Charles, haleluya, naam,

bwana, bila shaka, watu walioutikisa ulimwengu katika siku zao.

<sup>146</sup> Tunachohitaji leo hii sio tena... ambao ni akina mama na watu waliowekwa wakfu, wamtangulize Mungu. Jambo ndilo hilo. Tunatanguliza kila kitu kingine, “Vema, mimi ni mfuasi wa shirika hili *hapa* chini.”

<sup>147</sup> Loo, mimi ni mfuasi wa Shirika fulani, pia, liko *huko* juu. Mnaona, hilo ndilo Shirika la kushiriki, Shirika la Yesu Kristo, watu maskini, duni, waliotengwa, nina furaha sana naweza kusema mimi ni mmoja wao. Hiyo ni kweli. Nina furaha sana kuwa mfuasi wa Shirika hilo. Jitenge, toka ulimwenguni, usiwe mshiriki pamoja nao. Ibrahimu alijitenga, naye Mungu akambariki, na kumpa kila ahadi aliyompa, alimthibitishia hayo alipojitenga.

<sup>148</sup> Nawe unapojitenga na mambo ya ulimwengu, kutokuamini... Kuna dhambi moja tu, kuna dhambi moja tu, hiyo ni kutokuamini. Kuvuta sigara si dhambi, kufanya uzinzi si dhambi, kulitumia Jina la Bwana bure si dhambi, hizo ni sifa za kutokuamini, hiyo ni kwa sababu huamini, sababu ya wewe kufanya hivyo. Unaona? Dhambi ni kutokuamini. “Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa.” Hata huwezi kufikia msingi wa kwanza isipokuwa uamini kila Neno la Mungu, na kuita kitu kingine chochote Kwake kana kwamba ni uongo. Amina.

<sup>149</sup> Ee Mungu, laiti kungekuwa na njia fulani ningeweza—ningeweza tu kuwachukua watu, na kuyaweka kwenye gudulia, na kuyamimina kooni mwao, kisha kuyafungia ndani, ili yasiweze kutoka. Naam, bwana, ili kwamba waweze kuliaona. Simaanishi kuwa fidhuli, lakini ni—ninajaribu... Hii si, sikusema hivyo kwa mzaha, hapa si mahali pa mizaha, hii ni mimbara, hii ni nyumba ya Mungu, ni mahali palipowekwa wakfu Kwake, ambapo Injili na madhihirisho ya Roho Mtakatifu yanapaswa kujulikana.

<sup>150</sup> Sisimami hapa nipate kuonekana, ama kupiga makelele nipate kusikiwa, ni Roho Mtakatifu kupitia kwa Neno. Mnaona, hilo ndilo tunalotaka kufanya, ni kuwarudisha watu kwa Mungu tena, tuone watu kutoka mitaani na kutoka ulimwenguni, wakiingia katika nyumba ya Bwana, kwa utamu na utulivu katika Roho Mtakatifu, wakiabudu katika Roho, Roho Mtakatifu akitembea Kanisani kwa ishara na maajabu na karama.

<sup>151</sup> Loo, kila Neno ni imani. Kama wewe ndiye, kama wewe ni mwana na binti wa Mungu, hakuna hata Neno moja katika Biblia hii, ambalo ungeining'iniza nafsi yako juu Yake. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

“...niliombewa jana usiku, lakini unajua mkono wangu uliolemaa haujapata nafuu hata kidogo, hapana shaka niliukosa.” Huyu si mtoto wa Ibrahimu. Hapana.

<sup>152</sup> Wakati Sara, haikuleta tofauti yoyote, wakati alipokuwa na umri wa miaka sitini na mitano, hakuwa tena kama wanawake wanavyopaswa kuwa ambao watapata watoto, na mwezi wa kwanza, mwezi wa pili, mwezi wa tatu, badala ya Ibrahimu kudhoofika zaidi na zaidi, alipata nguvu zaidi na zaidi, amina, ikaendelea kupanda juu, “Loo, haleluya, utakuwa mkubwa kuliko ulivyowahi kuwa!” Mnaona? Mpaka miaka ishirini na mitano ikapita, miaka ishirini na mitano, naye alikuwa na nguvu zaidi mwishoni mwa miaka ishirini na mitano kuliko alivyokuwa huko nyuma wakati alipoanza. Alipata tu nguvu wakati wote, akisema, “Mungu asifiwe, andaa vijibuti, yuaja. Naam, bwana, ataninii, huyo mtoto atazaliwa.”

“Unajua je, ewe jamaa mzee?” Umri wa miaka mia moja, “Unajua je?”

“Mungu alisema hivyo.” Jambo ndilo hilo. Hiyo ni kweli.

<sup>153</sup> Sasa, kama sisi ni Uzao wa Ibrahimu, halafu tunasema, “Vema, niliombewa jana, bali sijapata nafuu,” loo, Uzao wa Ibrahimu, Uzao wa Ibrahimu! Mwaminini Mungu kwa Neno Lake. Mungu alifanya ahadi, Mungu hutimiza ahadi Yake, la sivyo Yeye si Mungu.

<sup>154</sup> Mungu alifanya ahadi ya kwamba angeonyesha ishara hizi katika siku za mwisho. Yeye anafanya hivyo kwa sababu gani? Basi watu watalikosoa, kama walivyofanya jana usiku. Wanapofanya hivyo, wanajitia muhuri milele mbali na Mungu, Yesu alisema hivyo, “Neno moja dhidi Yake halitasamehewa kamwe katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.” Mnaona?

<sup>155</sup> Na kitu kama hicho hakina budi kusonga mbele, ili kwamba Mungu... Mungu mwenye haki asingeweza kumwaga ghadhabu Yake juu ya watu wenye haki, haina budi kuwashukia watu wasioamini, wanaokataa. Ndivyo hasa. Ulimwengu hauna budi kuona kitu hicho kabla hawajaweza kukikataa, na kukikataa, basi Mungu ana haki ya kumwaga ghadhabu Yake. Hiyo ni kweli kabisa.

<sup>156</sup> Hiyo ndiyo sababu alifanya juu ya Israeli, nao wote wakafia mle ndani. Wakati—wakati Tito alipoingia, akauteka huo ukuta, mbona, damu ilitiririka hadi karibu kwenye lijamu ya farasi, walisema. Wanawake waliwaua watoto wao wenyewe na kuwala, wakala maganda ya mti, nyasi kutoka ardhini, Waisraeli, wafuasi wa kanisa, watu waaminifu, watakatifu, walilijua Neno vizuri sana. Lakini walifanya nini? Walishindwa kuamini Ishara ya kweli waliyopewa na Mungu, Masihi, nao wakailipia. Mungu alikuwa mwenye haki katika kufanya jambo hilo, utakatifu Wake unaihitaji. Hakuna haki bila adhabu.

<sup>157</sup> Vema, unasema, kama kuna taa nyekundu huko nje, ivuke hiyo taa nyekundu, “Hukupaswa kufanya hivyo,” hiyo si haki. Kuna adhabu ya kuvuka hiyo taa nyekundu, adhabu, unatozwa faini kwa sababu yake. Sheria bila haki si sheria, huna budi kuwa na haki, nao utakatifu wa Mungu unahitaji haki.

<sup>158</sup> Naye Mwanawe alilipa gharama kukukomboza, na kama ukikataa kuichukua, halafu uchukue baadhi ya ukanisa, ama *kitu fulani kingine*, maskini mambo ya nje ya kawaida, namna hiyo, huwezi kumlaumu Mungu. Taa nyekundu inaning’inizwa mbele yako, inaning’inia sasa hivi. Naam, bwana. Usiiruke hiyo, uko kwenye mstari wa hatari.

<sup>159</sup> Ninyi ni watoto wa Mungu, rudini kwenye agano lenu, rudini kwenye nchi ya ahadi. Ahadi ni nini? Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, “Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wale walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Ahadi ni kwa ajili yao. Naam, bwana.

<sup>160</sup> Sasa, tunaona wakati Ibrahimu alipojitenga, Mungu alimjia, akasema, “Ibrahimu, yote *haya* ni yako.” Sasa, kamwe hakuwa amesema jambo hilo hapo kabla. Lakini, mnaona, alikuwa angali amefungwa na mambo aliyoshikilia, uzi mdogo *hapa*, sehemu nyingi sana legev, alikuwa bado na Lutu, na wabishi, na kadhalika.

<sup>161</sup> Kwa hiyo basi wakati alipojitenga, akafika mahali ambapo Mungu kweli alimwambia aende, Ibrahimu, ndipo Mungu akamtokea, kasema, “Sasa, Ibrahimu, simama utembe kote nchini, iangalie, yote ni yako. Ninakupa uponyaji wa Kiungu, ninakupa wokovu, ninakupa ubatizo wa Roho Mtakatifu, ninakupa ahadi hizi zote, kila moja ya hizo ni yako, Ibrahimu. Zianganalie, uone yote uliyo nayo.” Mnaona? “Angalia tu kilicho chako. Sasa, yote ni yako, Ibrahimu.”

<sup>162</sup> Ninaweza kumwona baba Ibrahimu akiangalia tu, akisema, “Mungu asifiwe! Ninamiliki mlima *ule*, ninamiliki mlima *huu*, ninamiliki *kile*, ninamiliki *hiki*, ninamiliki *kile*, vyote ni vyangu.” Amina. Hivyo ndivyo ilivyo. Kila kitu katika Biblia ni mali yangu, mimi ni mwana wa Ibrahimu, mimi ni Uzao wa Ibrahimu, wewe ni Uzao wa Ibrahimu.

<sup>163</sup> Lakini, unaona, huna budi kuja kwenye chumba cha kubadilishia hundi kwanza. Jiweke sawa, rudi kwenye nchi ya ahadi, ambapo Roho Mtakatifu ni muziki mtupu moyoni mwako kila siku, nawe unaishi maisha, loo, jamani, utukufu wa Mungu ukikumwagia utamu wa Bwana Yesu. Loo, hilo ni halisi. Ndipo basi, *kitu fulani* moyoni mwako kinakushikilia, “Nanga yangu inashikilia,” una *kitu fulani* hapa nje kinachokuvuta, unajua unachochewa vizuri.

<sup>164</sup> Angalia Biblia, angalia jinsi wewe...yale waliyofanya katika siku hiyo, angalia nyuma uone kama mambo yale yale yako pamoja nawe, uone kama tukio lile lile walilokuwa nalo

huko nyuma ndilo tukio lako. Kama ndivyo, basi yote ni sawa, omba tu lolote utakalo, dumu moja kwa moja katika Neno, omba utakalo, utapewa.

<sup>165</sup> Sasa, ninataka kuendea kifungu kimoja zaidi. Sidhani tutakuwa na wakati wa kukifikia hicho kingine, nitakipata, labda, kesho usiku. Hapa ni mahali pengine ninapotaka kupaendea, baada ya kule kutengana, katika mlango wa 14, tunaona jambo kuu, la kipekee kabla ya kuthibitishwa kwa lile agano. Labda nitalipata kesho usiku.

<sup>166</sup> Lakini kule kuthibitishwa kwa lile agano, sasa, Ibrahimu alitoka nchini, hakika, akavuka mto Frati, wengi wenu mlivuka, mkabatizwa, mkaingia nchini. Sasa, msirudi moja kwa moja Misri, kaeni mumu humu nchini, tiini, dumuni moja kwa moja katika ahadi ya huyu Baba, mnaona. Dumuni moja kwa moja chini ya Roho Mtakatifu, haidhuru. . .

<sup>167</sup> Usijifananishe na mtu fulani wa ulimwengu, wewe jifananishe na Yeye. Unaona? Mwangalie, angalia maisha Yake. Usitende kama *Fulani-wa-fulani* atendavyo, Dada Susie, ama Ndugu Jackson, ama yeyote yule, usi—usionekane kama, usitende kama wao, wewe tembea tu pamoja na Yeye. “Ijaze njia yangu kila siku na upendo, ninapotembea na Hua wa Mbinguni.” Dumu tu moja kwa moja pamoja Naye, angalia jinsi inavyokufanya mtamu, na kuukatilia mbali ulimwengu wote. Loo, jamani, hujali watu wanasema nini, unatembea pamoja na Mungu.

<sup>168</sup> Hapa si muda mrefu uliopita, mimi na mke wangu tulienda kwenye duka la vyakula, nasi tulikuwa nchini mwangu. Mimi. . . Loo, bila shaka, hawangefanya hivyo huku California, lakini huko nchini mwangu. . . Sisi. . . Nilikuja kutoka mahali fulani nilipokuwa, ninaamini, huko nje visiwani, Visiwa vya Karibea. Nikarudi, naye akasema, “Vema, Mpenzi, nina furaha uko ndani,” kasema, “inatubidi kwenda dukani,” kasema, “kununua vyakula.”

<sup>169</sup> Nikasema, “Vema, tutaondoka.” Ndipo nikatoka nje na kukanyaga maskini lile gari la kale, na—na kwa hiyo tukaanza safari, tukashuka. Vema, nikaendelea, nami ningeona, nami. . . Ni—ni—nikaangalia, na baada ya kitambo kidogo, tuliona moja ya vituko vya ajabu sana ambavyo tulikuwa tumeona, ilikuwa mnamo Julai, Agosti, kitu kama hicho, katika nchi yetu, nilimwona mama mmoja aliyekuwa amevaa gauni. Nami nikawaza, “Si ni ajabu hiyo?” Mnaona? Alikuwa amevaa gauni. Wote walikuwa, walikuwa wamevaa kaptura ndogondogo, iwe walikuwa waja wazito au la, walitembea huku wamevaa hizo. Na—na baadhi yao. . .

<sup>170</sup> Akasema. . . Nikasema, “Angalia, hilo si—hilo. . . ? Hivi yeye haonekani kama mama wa heshima? Amevaa sketi.” Nikasema,

“Hiyo si ni ajabu? Sijamwona mmoja tangu niliporudi, sidhani.” Mnaona? Nami nikasema, “Si ni bu- . . .?”

<sup>171</sup> Akasema, “Bill, nataka kukuuliza jambo fulani.” Akasema, “Sasa, unajua yule msichana aliyesimama pale pale pembeni, unajua mahali alipo, huenda kanisani, unajua.”

Nikasema, “Um-hum.”

“Vema,” kasema, “ni kwa nini kwamba—kwamba sisi . . .? Wao—wao ni—wao ni watu kama tulivyo sisi.”

Nikasema, “Hakika, kama tu tulivyo, hasa.”

<sup>172</sup> Akasema, “Vema, kwa nini—ni kwa nini hawaninii . . .? Wao ni—wao—wao ni wa kidini, wanaenda kanisani, na mambo kama hayo.” Kasema, “Ni kwa nini kitu fulani ndani yetu hakituruhusu kufanya hivyo?”

Nikasema, “Vema, sisi ni—sisi ni . . .”

Akasema, “Mbona, wao ni Wamarekani tu, kama tulivyo sisi.”

Nikasema, “Hivyo ndivyo ilivyo, wao ni Wamarekani, sisi sio.”

Akasema, “Ati nini?”

Nikasema, “La, sisi si Wamarekani, la.”

<sup>173</sup> Ukienda Ujerumani, unapata roho ya Kijerumani. Unaona? Ujerumani ina roho ya kitaifa. Ukienda Uswidi, unapata roho ya Kiswidi.

<sup>174</sup> Sasa, nilipokuwa Ujerumani tulikuwa na, Ndugu Arganbright yupo hapa mahali fulani, nasi tulikuwa na mkutano mkubwa, tulikuwa na wastani wa waongofu elfu kumi kila usiku, nao waliandikisha Wajerumani elfu hamsini siku tano usiku, wakomunisti, na kadhalika, wakimjia Kristo. Ndipo ningeshuka kwenda mtaani, na hawa hapa watakatifu wakiwa na bilauri kubwa mno ya pombe mikononi mwao, wakipiga makelele, “Utukufu! Haleluya! Bwana asifiwe.”

<sup>175</sup> Nami nikaenda kule kuketi mezani, nyumba ya watakatifu, ya kitauwa, nao wote walikuwa wamemwagiwa pombe hiyo, nikawaza, “Jamani!” kote namna hiyo.

<sup>176</sup> Nao, kwa hiyo nilikuwa nikila, wote wakaanza kuzungumziana Kijerumani, wakaniangalia, naye Daktari Guggenbuhl akasema, “Wanashangaa ni kwa nini hunywi pombe yako.”

<sup>177</sup> Ndipo nikawaza, “A-ha.” Nikasema, “Wewe sema ninayosema.” Akasema . . . Nikasema, “Nadhani ni sawa,” nikasema, “lakini, mnaona, nilizaliwa Mnadhiri, sikupaswa kuvuta sigara, kutafuna tumbaku, wala kunywa chochote.”

Loo, hilo lilikuwa sawa, “Mungu asifiwe,” wakaendelea tu kunywa moja kwa moja. Hiyo ni Ujerumani.

<sup>178</sup> Nikaenda Italia, hawatakupa maji, ni divai. Basi nikaenda kwenye duka la dawa na kujinunulia baadhi ya maji haya yaliyotoneshwa, yalikuwa kwenye jagi, ilikuwa imezungushiwa moja ya vitu kama mirija. Nadhani kila mtu alidhani nimebeba ya aina yangu mwenyewe. Kwa hiyo nilizunguka tu huku nikiyanywa kutoka kwenye jagi hili wakati wote, mnaona, bali yalikuwa ni maji yaliyotoneshwa. Sikutaka divai yao, la. Lakini, mnaona, hiyo ni—hiyo ni roho ya Kiitaliano.

<sup>179</sup> Kisha ukienda huko Ufini, nilikuwa huko, nao walitupeleka huko kutoa, walisema, “Tunashuka kwenda kwa YMCA na—na kuwa na sauna.” Huko ni kuoga kwa Wafini.

<sup>180</sup> Nilipofika huko chini, nilifikiri kitu fulani kilisikika cha kigeni sana, nikasema, “Siamini ninataka, kuoga.” Na *kwa namna fulani* wakati hao ndugu wote waliingia mle, huyu hapa anakuja maskini mwanamke mwenye nywele za shaba akiwa na lundo kubwa la taulo, akizunguka mahali hao wawanaume walipokuwa wamevua nguo, Nikasema, “Hei, hei, usifanye hivyo!”

<sup>181</sup> Naye akaniangalia, kidogo akacheka, akaingia ndani. Nao hawa hapa huko nje huku hao wanawake wakiwasugua hao wanaume huko nje, nikamwambia Daktari Manninen, nikasema, “Hilo si sawa.”

“Loo,” akasema, “wao ni wanawake wa kusugua tu, kama wauguzi wenu wa Kimarekani, kitu kama hicho.”

Nikasema, “Sijali ni nini, Mungu kamwe hakukusudia iwe hivyo.” Hiyo ni kweli, lakini hiyo ni Ufini. Mnaona?

<sup>182</sup> Halafu unakuja Marekani... Wakati mimi... Kuna mtu yeyote aliyewahi kuwa huko—huko Ulaya katika Rumi, kisha akashuka kwenda Sant’Angelo? Ni fedheha kwa taifa letu, hata huko Italia, lina bango, papo hapo karibu na makaburi ya Sant’Angelo, kasema, “Wanawake wa Marekani, tafadhali vaeni nguo kuwaheshimu wafu mnapoingia hapa.” Loo, jamani!

<sup>183</sup> Mimi na Ndugu Arganbright tulikuwa tumeketi pale tukila, tukiendelea vizuri sana na mnofu mzuri, mpaka ilipotokea Binti wa Marekani alijitokeza akiwa na vito vya kutosha mikononi mwake kwa ajili ya duka hili la malimali, sigara imetokeza yapata umbali *huo*, na miwani imetokeza namna *hii*, akiwa na mbwa wa pudeli, na akamketisha mezani. Loo, inakufanya uone aibu, taifa linalodhaniwa kuwa ni taifa la Kikristo!

<sup>184</sup> Hilo halilifanyi la Ukristo. La, bwana. Sisi si Wamarekani, tunaishi hapa, kama taifa, wanadamu, tunaishi chini ya hili, ndilo taifa kuu kuliko yote ulimwenguni, kuhusu hilo, lakini ninawaambia, kama tu Joan wa Arc katika ule wakati wa mapinduzi ya Ufaransa, Ufaransa ilihitaji mapinduzi, lakini basi ilihitaji mapinduzi-badilifu, hayo ndiyo Marekani inayohitaji, inahitaji uamsho na uamsho-badilifu, hiyo ni kweli, kunyosha baadhi ya mambo yaliyo makanisani na maishani mwa

hao watu. Demokrasia ni sawa, lakini basi tunahitaji uamsho katika demokrasia ili kuinyosha, hiyo ni kweli kabisa. Loo, kama sisi ni Wamarekani, kama . . . tumezaliwa Wamarekani huru, kile tunachoshukuru kwa ajili yake.

Nikamwambia mke wangu, “Lakini, unaona, tunatoka Nchi nyingine, Mpenzi.”

Akasema, “Nchi gani nyingine?”

<sup>185</sup> Nikasema, “Kutoka Mbinguni, tumezaliwa kutoka Juu. Kwa hiyo, huko juu. . .” Nikasema, “Wamarekani? Hakika, kila mtu hufanya hivyo. Wanatoka nje, wanavuta sigara, wanavaa nguo za kizinifu, wanaume wanawapigia mbinja na kuwafanyia yasiyofaa, na kuwakodolea macho, na kusababisha ajali, na kadhalika,” nikasema, “hao ni Wamarekani.” Hiyo ni kweli. Hao ni Wamarekani, koho. Mnaona? Hiyo ni kweli.

<sup>186</sup> Wanatoka wakikodoa macho, wachafu, wenye vinyaa, waovu, tabia mbaya, wanaenda kanisani, mashemasi, hata wahubiri. Naam, hiyo ni kweli. Wanaingia kanisani, na kutenda- . . . wanajiita Wakristo, na kutenda hivyo? Ni kitu gani kinachotukia? Wao ni Wamarekani, hiyo ni roho ya Marekani.

<sup>187</sup> Kwa nini unakaa nyumbani usiku, ukiangalia vichekesho kwenye hiyo televisheni ambavyo havipaswi kutajwa kwenye kundi la mabaharia walevi, vipindi visivyokaguliwa, na upuuzi wote mchafu wa namna hii? Baadhi ya akina mama na akina baba wazee waliokaribia kufa, na kuwapa televisheni wakae nyumbani wasiende kanisani. Wanachohitaji ni kurudi kwenye mkutano wa maombi, wamrudie Mungu. Kweli. Si ajabu tuko tayari kuwa na bomu la atomiki likiwa na jina letu juu yake, hakika tunalistahili. Hiyo ni kweli kabisa. Tumekosea, na tumemtendea Mungu dhambi. Mungu anaweza kumtuma Roho Wake Mtakatifu kote nchini. . .

<sup>188</sup> Hapa si muda mrefu uliopita katika mji wetu kulikuwa na mwanamke aliyekuwa akizunguka, alikuwa na m—mvulana mdogo, alikuwa akizunguka-zunguka, naye alikuwa katika duka la malimali, naye angetikisa vitu vidogo, kasema, “Unakiona, Mpenzi? Unakiona, Mpenzi?” Maskini mtoto huyo aliketi tu na kukodoa macho, akakodoa macho. Kasema, “Unakiona, Mpenzi? Angalia hapa, hiki si kinapendeza? Unakiona?” Maskini mvulana huyo alikodoa macho tu. Hatimaye, alishtuka sana akaanguka kwenye kaunta.

<sup>189</sup> Baadhi ya watu dukani walienda kuona shida yake. Kasema, akasema, “Loo, la, haiwezi kuwa sawa.” Kasema, “Maskini mvulana wangu,” akasema, “amekuwa tu, alipatwa na shida fulani yapata mwaka mmoja uliopita, naye anaketi tu na kukodoa macho. Na chochote kinachopaswa kuvutia usikivu wa mvulana mdogo wa umri wake, hakimvutii, tena.” Kasema, “Yeye huketi tu na kukodoa macho.”

<sup>190</sup> Kisha kasema, “Sasa, daktari alisema amepata nafuu, lakini,” kasema, “sivyo, ninaweza kumwonyesha vitu ambavyo kweli mvulana mdogo anapaswa kuvutiwa navyo,” kasema, “haoni hilo,” kasema, “anakodoa macho tu.”

<sup>191</sup> Hivyo ndivyo tu kanisa limefanya. Mungu ametuma kila karama kanisani inayoweza kuwaziwa, amekuwa na Oral Roberts, Billy Graham, na kila namna ya ishara na maajabu; nalo kanisa linaketi tu na kusema, “Vema, mimi ni mfuasi wa *hili*, hata hivyo, mnaona,” linaketi tu na kukodoa macho. Kuna kasoro, kanisa lina kasoro kiakili, kiroho. Naam, bwana.

<sup>192</sup> Ninyi ni—ni wa kilimwengu sana, kama kuku, sio tai, kuku chini ardhini, vifaranga vya ardhini, mkichakura kwenye kitalu, bila kula chakula cha tai cha angani, ndege wa mbinguni. Mnaona? Lakini kanisa limekuwa kama kuku, limefikia mahali ambapo ni ulimwengu tu, na mambo ya ulimwengu, likimeza upuuzi kama huo, kuingiza kanisani, na dini ya kijamii, na kila . . . Loo, ni mbaya sana!

<sup>193</sup> Huenda msinipende baada ya haya, lakini, ndugu, kwenye Siku ya Hukumu damu yenu haitadondoka kutoka mikononi mwangu, na hilo ni jambo moja, hiyo ni kweli, mtajua ukweli. Fanyeni nao chochote mtakacho, ni kwa ajili yenu. Lakini wewe . . . hiyo ni . . .

<sup>194</sup> Nikasema, “Wenyeji wa Ufalme wa Mbinguni wamezaliwa kutokana na Roho aliye *huko* juu, si kutoka *hapa* chini.”

<sup>195</sup> Awe ni Myahudi, Mfaransa, Mmarekani, ama yeyote yule, wao si wa ulimwengu huu, wao ni wenyeji wa Ufalme ule. Kwa kuwa sisi tunaokiri kuwa ni Wakristo, tunatangaza waziwazi ya kwamba tunautafuta Mji, ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu. Tunautazamia Ufalme ujao. Nasi tunakiri kuwa wasafiri na wageni katika ulimwengu huu, tukizunguka-zunguka, tukiutazamia Ufalme huo uje duniani kama ulivyo Mbinguni, tukitazamia kutimizwa kwa ahadi za Mungu, Uzao wa Ibrahimu.

<sup>196</sup> Ibrahimu alijitenga na mambo yote ya ulimwengu, na kutembea katika nchi ya kigeni, akikiri kwamba alikuwa msafiri, mgeni. Hakuwa wa mahali hapa, alikuwa akiutafuta Mji huo, naye akazunguka-zunguka katika majangwa na kadhalika, akiutazamia huo Mji. Na kila Uzao wa Ibrahimu anafanya jambo lile lile, akiweka kando kila mzigo, na kukiri ya kwamba sisi ni wasafiri. Sisi si wafuasi wa kanisa, sisi ni wasafiri. Hatutendi kama ulimwengu, sisi ni wasafiri na wageni, tunatenda kipekee kwa mambo ya ulimwengu. Tunautafuta Mji, ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu.

<sup>197</sup> Ninakuuliza, rafiki Mkristo, nakuuliza, ewe rafiki mwenye dhambi, vipi kama ulikuwa unakufa usiku wa leo, Marekani ingeweza kukuokoa? Utakuwa wapi miaka elfu kumi tangu usiku wa leo? Utakuwa wapi, labda, utakuwa wapi asubuhi?

Kikomo chako huenda kimetiwa muhuri usiku wa leo, hujui. Hebu niwaonye, mjipatanishe na Mungu. Pateni roho... Fahamianeni na mambo ya Mbinguni ya huyo Roho anayeshuka kutoka Mbinguni ambako utakatifu unasimama, ambako Malaika wa Mungu wanasimama, ambapo Yesu Kristo amesimama mkono wa kuume wa Mungu katika ukuu, na utukufu, utakatifu, na nguvu za Mungu, ndipo unatembea kama mgeni hapa, kwa sababu wewe ni mgeni hapa, wewe si wa ulimwengu huu.

<sup>198</sup> “Ninyi si wa ulimwengu huu, watoto wadogo, wala mimi si wa ulimwengu huu. Ninawaombea.” Mnaona, Yesu akiliombea Kanisa Lake, kwamba wasiwe wa ulimwengu. Wao si wa ulimwengu, Sijali, wewe si Mmarekani, wewe si Mswidi, wewe si Mzungu, wewe ni Mkristo. Na kama wewe ni Mkristo, roho yako inatoka Kule juu, kwa hiyo inakufanya uishi kitakatifu, utake kuwa mtakatifu, utake kutenda kama Kristo, kutenda kama Mungu. Shauku yako yote iko Mbinguni, wala si wa ulimwengu.

Wazo moja zaidi, tafadhalini, kidogo tu. Tuna dakika kumi kamili tupate kutoka kwa wakati unaofaa.

<sup>199</sup> Basi ilikuwaje kwa Lutu alipojichagulia? Nini kilitukia? Machafuko yalianza mara moja. Ilikuwa ni kitu gani? Wafalme fulani walishuka na kumchukua Lutu mateka, na kumchukua, Sodoma, na kuwachukua wake zao, na kuchukua kila kitu, na kuondoka nacho.

<sup>200</sup> Mwangalieni Ibrahimu katika mlango wa 14 sasa, Roho wa Kristo aliyebarikiwa juu yake, alimfuatilia ndugu yake aliyeanguka. Roho wa Kristo juu ya Ibrahimu, alimfuatilia ndugu yake aliyeanguka, na kumrudisha. Ibrahimu, mhubiri wa haki, alimfuatilia ndugu yake aliyeanguka, yule ndugu wa kimadhehebu, na kumrudisha. Akamrudisha kusudi apate nafasi nyingine, baada ya Shetani kumtoa, akamrudisha apate kuwa na ushirika tena.

<sup>201</sup> Basi Lutu alichukua wa—wazo gani kuu kulihusu? Je, alitoka na Ibrahimu akisema, “Baba Ibrahimu, nimekosea. Ninajua sasa, nimekosa baraka, nilijisahau huko nje, nikatoka nikaingia ulimwenguni. Sasa, nimeninii... Ninajua—najua u—umenirudisha, ninathamini jambo hilo. Nitaenda na kushika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa.” La, alishuka moja kwa moja akarudi Sodoma tena, na huko, kumechafuka, akaingia Sodoma. Hiyo ni kweli?

<sup>202</sup> Lakini mwangalie Ibrahimu, katika kufunga tu sasa, lilikuwa ni jambo zuri jinsi gani! Ibrahimu aliporudi kutoka kuwapiga hao wafalme, angalieni kilichotukia: Melkizedeki alitoka kwenda kumlaki. Melkizedeki, ambaye alikuwa Mfalme wa Salemu, Mfalme wa amani, Mfalme wa haki.

<sup>203</sup> Yeye alikuwa ni nani? Hakuwa na baba, hakuwa na mama. Yeye hakuwa Yesu, maana Yesu alikuwa na baba na mama pia.

Lakini Mtu huyu hakuwa na baba, hakuwa na mama. Ukitaka kufuatilia hilo, chukua Waebrania, mlango wa 7. Hakuwa na baba, hakuwa na mama, kamwe Uhai haukuanza, wala kamwe Uhai haukuisha. Alikuwa Mfalme wa Salemu, ambaye alikuwa Mfalme wa Yerusalemu, ambaye ni Mfalme wa amani, ambaye ni Mfalme wa haki. Hana mama, hana baba, hana wazazi, hana mwanzo wa miaka, wala mwisho wa Uhai.

<sup>204</sup> Alikuwa ni Mungu, hakika alikuwa. Alishuka katika mfano wa Melkizedeki, naye akakutana na Ibrahimu (Angalieni, hii ni sehemu nzuri.) baada ya vita kwisha.

<sup>205</sup> Ibrahimu, mhubiri wa haki, alikuwa ameingia katika watu wa kawaida, na—na huko nje katika jambo lisilo la kitauwa, na kumnyakua ndugu yake, kumrudisha, “Rudi, Ndugu, rudi!” Je, ilifaidi uamsho wa Ibrahimu chochote? La, Lutu alirudi moja kwa moja huko Sodoma tena, huko akaangamia katika aibu pamoja na binti zake, na kadhalika, aliangamia huko.

<sup>206</sup> Lakini baada ya Ibrahimu, yule mkweli, mwenye haki wa Mungu, alipokuwa amepata uamsho, na baada ya vita kwisha, Melkizedeki akakutana naye, naye Ibrahimu akampa sehemu ya kumi ya nyara. Naye Melkizedeki alimpa nini? Divai na mkate, Ushirika, baada ya vita kwisha.

<sup>207</sup> Yesu alisema, “Sitaula pamoja nanyi tena, mpaka nitakapokula huu upya pamoja nanyi katika Ufalme wa Baba Yangu.” Vita vitakapokwisha, mtumishi wa Mungu, siku moja Melkizedeki, Mfalme mkuu wa amani, Mfalme mkuu wa Mbinguni, bila baba, bila mama, bila mwanzo wa Uhai, wala mwisho wa Uhai, ama, bila mwanzo wa siku, wala mwisho wa Uhai, Yeye atatulaki baada ya vita kwisha, na kutupatia Ushirika.

<sup>208</sup> Loo, enyi Uzao wa Ibrahimu, nawatakia heri. Hivi huna furaha kwamba unaweza kuwa Uzao wa Ibrahimu, mtumishi wa Mungu akipigana na mambo ya ulimwengu? Na, loo, jinsi inavyofanya moyo wako kujisikia kuona kanisa lile lile unalopenda likiangukia ulimwenguni! Nawe ulilinyoshea mkono, na kulivuta, namna *hiyo*, na kujaribu kulitikisa, na kulionyesha, litarudi moja kwa moja kwenye kitu kile kile. Mnaona? Lakini kumbukeni:

Vita vitakapokwisha, tutavaa taji!  
Tutavaa taji! Naam, tutavaa taji!  
Basi vita vitakapokwisha, tutavaa taji  
Katika Yerusalemu mpya.  
Kuvaa taji, kuvaa taji,  
Kuvaa taji angavu na inayometameta.  
Basi vita vitakapokwisha, tutavaa taji  
Katika Yerusalemu mpya.

<sup>209</sup> Huko chini Kentucky, nilikotoka, Kanisa la kale la Kimishenari la Kibatisti, tofauti pekee niliyoona kati yao

na Pentekoste ilikuwa ni ushahidi wa kwanza, kunena kwa lugha. Ningewaona hao akina mama wazee, wamevaa zile kofia za kale, namna hiyo, na maskini pini za nywele juu ya nywele zao, na namna hiyo. Wangesimama pale, na kusimama na kuimba huo, wakipembeza maskini kofia hizo, machozi yakitiririka mashavuni mwao, na kupiga mayowe na kulia na kuona maono ya Mungu. “Vita vitakapokwisha, tutavaa taji!” Wanangojea kule kwenye lile tundu la kale usiku wa leo, mahali fulani huko chini kwa ajili ya ufufuo, kwa kuwa:

Katika ile asubuhi angavu na isiyo na  
mawingu wakati waliokufa katika Kristo  
watakapofufuka,  
Na kushiriki utukufu wa kufufuka kwake;  
Wakati waliookolewa wa duniani  
watakapokusanyika Upande ule mwingine,  
Majina yaitwapo huko juu. . .

210 Ninataka kuonyesha alama za vita. Ninataka kuninii. . . Hivi hutaki kusaidia kumfanya mtu fulani aoko?

211 Wakati mmoja Kaisari alikuwa anaenda kufanya karamu kubwa na gwaride kubwa, naye akasema, “Ninataka kuleta mtu mwenye heshima aketi karibu nami tupande farasi.” Maofisa wote wakasugua ngao za—zao, na kukata manyoya yao, na kufanya panga zao zimetamete sana, nao wakatembea karibu na Kaisari namna *hii*, wamevaa mavazi yao makubwa ya kimadhehebu, wakipita namna hiyo, “Kaisari, unaona mimi ni nani?” Kaisari aliketi na kuwaangalia, akawaangalia.

212 Mara maskini mtu wa miguu akapita amepondwa sana na ana makovu, kidogo ameinamisha kichwa chake. Kaisari akasema, “Hebu kidogo. Njoo hapa.” Kasema, “Kwani unafanya nini umejaa makovu namna hiyo.” Kasema, “Ulipata wapi makovu hayo?”

Kasema, “Huko nje kwenye uwanja wa vita, nikikupigania.”

Kasema, “Panda hapa juu, wewe ndiwe utakayeendesha karibu nami.” Hiyo ni kweli.

213 Paulo alisema, “Ninachukua mwilini mwangu chapa za Yesu Kristo.” Vita vitakapokwisha, wakati ninii yetu. . . siku moja tutahubiri mahubiri ya mwisho, tufunge Kitabu kwa mara Yake ya mwisho, tumbwe wimbo wa mwisho, tuombe maombi ya mwisho, na ndipo basi, vita vitakwisha kwangu siku moja, vita vitakwisha kwako, usiwe na wasiwasi wowote, kwa sababu basi tutakutana na Melkizedeki, yule Kuhani Mkuu mashuhuri, yule Kuhani Mkuu mashuhuri wa Mungu, Bwana wetu Yesu Kristo, Yeye atakayetupatia Ushirika, atuketishe chini baada ya vita kwisha. Wakati ukiwepo, hebu na tuwanyakue hao Lutu, na kadhalika, tuwezao, na kujaribu kuwavuta watoke Sodoma, kwa sababu ha—hatuna budi kufanya hivyo.

214 Bwana na awabariki tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu wa maombi. Huku mmeinamisha vichwa vyenu na macho yenu yamefumbwa, ningetaka kuwaulizeni swali moja aminifu, niwaulizeni tu jambo moja: Je, wewe ni Mkristo? Kama sivyo, waweza kuinua mkono wako? Useme, “Ndugu Branham, nimeanguka kando ya njia, ningetaka kumrudia Mungu. Ningependa ku—ningetaka kufanya upya ushirika wangu. Nimeshuka kwenda Misri, mimi—mimi ni... ninataka kufanywa upya, nataka kurudi katika nchi ya ahadi. Niombee, Ndugu Branham, usiku wa leo, unapofunga.” Mwaweza kuinua mikono yenu? Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Kwenye roshani? Mungu...

215 Kuna mtu fulani huko juu kwenye roshani angesema, “Ndugu Branham, wakati mmoja nilipata ushindi, wakati mmoja nilikuwa mtu mtauwa, lakini *kwa namna fulani* magugu, na miiba, na kadhalika imenisonga, siko mahali ninapopaswa kuwa, ninajua siko, niombee, Ndugu Branham”? Vema. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Kunaweza kuwa na mwingine?

216 Kuna mmoja hapa ambaye hajawahi kumsimamia Kristo, asiyejua lolote kuhusu kuzaliwa mara ya pili, kamwe hajampokea Roho Mtakatifu, wewe si mwana wa Mungu, na unajua kama Mungu angekuja usiku wa leo, amtume Yesu duniani, kwamba hakika hutaenda pamoja Naye katika Unyakuo, nawe unataka kukumbukwa katika maombi kama mwenye dhambi? Waweza kuinua mikono yako, na kusema, “Niombee, Ndugu”? Mungu akubariki, ewe jamaa mdogo. Mungu akubariki. Hilo ni zuri, hilo ni sawa. Mungu akubariki. Kuna mwingine ungeinua mkono wako, useme, “Niombee, Ndugu Branham, si—sitaki kuuacha ulimwengu huu namna hii”?

217 Sasa, angalia, haidhuru utafanya nini maishani, huna budi kuliacha papa hapa duniani, ni kile tu unachotuma mbele yako, Utukufuni, kinachojalisha. Na kama wewe si Mkristo, kwa nini angalau usiinue tu mkono wako?

218 Nilimwona mvulana tineja, moja kwa moja wakati huu, zilipo njia panda za maisha, wakiinua mkono wao, “Ninataka kumjua Yesu kama Mwokozi wangu.” Ombeni Mungu atafanya mhubiri kutoka kwa mvulana huyo.

Ninamwona msichana mmoja huko nyuma akiinua mkono wake, msichana tineja tu.

219 Papo hapo wakati kila kitu, papa hapa katika machafuko ya msongamano huu wa dhambi na upumbavu wa ulimwengu, na hata hivyo kijana mwanamume na kijana mwanamke wakiinua mikono yao, “Ninataka kumjua Yesu kama Mwokozi wangu.” Hmm! Roho Mtakatifu anawajua walio Wake. Sasa, usingeweza

kufanya hivyo, Ndugu, wala usingeweza kulifanya, Dada, bila Mungu kusema nawe, kuna *jambo fulani* pale.

220 Sasa, kumbuka, ulipoinua mkono wako, ulivunja kila kanuni ya kisayansi ambayo sayansi iliwahi kuwa nayo. Sayansi inasema ya kwamba mikono yako haina budi kuning'inia chini, nguvu za uvutano zinaishikilia mikono yako chini, kama vile zinavyokushikilia chini duniani. Kwa hiyo ulipoinua mkono wako, hiyo ilionyesha ya kwamba kulikuwa na roho fulani ndani yako ambaye angeweza kuziasi nguvu za uvutano, kuna roho ndani yako iliyofanya uamuzi, "Nataka kumjua Kristo," ndipo mkono wako ukainuliwa kuelekea kwa Muumba wako.

221 Usingeweza kufanya hivyo pasipo Yeye kusimama karibu nawe, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba watakuja Kwangu; na yeyote ajaye Kwangu sitamtupa nje kamwe. Nitampa Uzima wa milele, na kumfufua katika siku ya mwisho." Ni ahadi ya jinsi gani! Kile ulichofanya ulipoinua mkono wako, kilikuwa ni kwa ajili ya Mungu.

222 Sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa ajili ya maombi, kama ukijisikia kuongozwa kumkaribia Mungu zaidi kidogo, kama ungetaka tuombe pamoja nawe, kama ukiangalia, na utaona katika ibada za uponyaji, huku Yeye akijua mioyo ya watu, anawafanya vipofu kuona, viziwi kusikia, viwete kutembea, anawapa wokovu, Yeye ni Mungu yeye yule, usiku wa leo. Je, utakuja hapa madhabahuni? Ungeweza kuja hapa, na kusema, "Ndugu Branham, sasa ninamkubali, jambo kuu zaidi ambalo lingeweza kufanywa, ninataka kumkubali Kristo kama Mwokozi wangu," tunapoomba?

223 Baba yetu wa Mbinguni, Neno ni kali, kweli, Bwana, na linakata, bali watu wameketi tu kwa subira na kwa utamu. Na, Baba Mungu, nikiweka msingi huu kuwafanya hawa Wakristo wajue ya kwamba hawajapoteza agano lao, walipewa bila masharti, bali watapoteza thawabu yao wasiporudi katika nchi ya ahadi.

224 Walipoteza furaha, ulimwengu ukaanza kunyemelea kanisani, tunaona jinsi unavyoendelea. Na ni kulingana na Neno Lako, hakuna njia tunayoweza kuukomesha, Baba. Lakini tunajaribu kuwapata wale walio tayari kuja, kwa kuwa tunaamini huu ndio wito wa saa kumi na moja, kilio cha usiku wa manane kinakaribia kutolewa. Sayansi inasema ni chini ya dakika tatu ifike usiku wa manane, wakati ulimwengu mzima utakapolipuliwa vipande-vipande. Vipi kama mshupavu fulani angeachilia moja ya hayo mabomu usiku wa leo, nalo lingeingia kwenye moja ya skrini za rada? Kila taifa ulimwenguni lingeachilia mabomu. Ulimwengu hauwezi kustahimili hilo, Baba.

225 Lakini kabla hili halijatukia, Wewe ulitoa ahadi ya kwamba tutakuwa tumeondoka. Kwa hiyo kama ingeweza kutukia kabla ya asubuhi, Sputniki, na ulimwengu ungeweza kufikia mwisho wake, katika dakika moja tu, nasi tunalionga kisayansi, basi kama liko karibu hivyo, kule Kuja kumekaribia kiasi gani? wakati kutatukia kabla ya hapo, kule Kunyakuliwa kwa Kanisa. Haitatubidi kusimama kwenye hukumu, Wewe uliilipia hiyo kwa ajili yetu. Tuko ndani Yako, huru na hukumu, “Nitakapoiona ile Damu, nitapita juu yenu.”

226 Baba Mungu, libariki Kanisa lako, na kuwafanya wajue ya kwamba—ya kwamba tunajaribu kwa moyo wetu wote kuona Kanisa halisi la Kipentekoste, limejazwa na Roho wako, likifanya miujiza na ishara. Wengi wao wameinua mikono yao usiku wa leo, wakishuhudia kwamba walikuwa wameanguka kutoka kwenye njia ya kale. Ninaomba, Baba, ya kwamba utawarudisha, usiku wa leo, kutoka Misri, kutoka kwenye vitunguu saumu na liki za Misri, wakale Chakula cha Malaika huku nje jangwani pamoja na Mungu. Tujalie, Baba. Tuko safarini kwenda Utukufuni.

227 Ninaomba, Baba, kwa ajili ya kijana huyu mwanamume na kijana mwanamke walioinua mikono yao usiku wa leo, mvulana huyu tineja na msichana tineja. Ee Mungu, hiyo mioyo myororo, ninaomba ya kwamba utawanyakua kutoka kwenye mioto ya Milele. Tujalie, Bwana. Jalia waje Kwako kwa utamu, na kuyatoa maisha yao Kwako. Tujalie, Bwana, hao ni wako. *Kwa namna fulani* maneno makali na magumu yaliyohubiriwa usiku wa leo, nikiamini kwamba niliongozwa kufanya na kusema yale niliyofanya na kusema kwa ajili. . . kwa Roho wako, ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utawabariki sasa, na jalia waje Kwako kwa utamu. Tujalie, kupitia Yesu Kristo.

228 Tunapoendelea kuinamisha vichwa vyetu, ninataka kuimba pambio moja, *Ninaweza Kumsikia Mwokozi Wangu Akiita*. Na sasa kama unataka kuja hapa, na kuturuhusu kuomba pamoja nawe kibinafsi, tutafurahia kufanya hivyo. Endelee ni tu kuinamisha vichwa vyenu, Wakristo wote wanaojua jinsi ya kuomba, ombeni.

Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita,  
Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita,  
Ninaweza kumsikia Mwokozi wangu akiita,  
“Itwae msalaba wako, unifuata, unifuata  
Mimi.”

Aniongozako ni . . .

Utafanya hivyo? Utakuja hapa juu pamoja na mzee huyu?

Aniongozako nitafuata,  
. . . aniongoza nitafuata,

Rafiki mwenye dhambi, utakuja?

... aniongoza nitafuata,  
Nitaambatana Naye, pamoja Naye kotekote.

Aniongozako...

<sup>229</sup> Mtakuja? Pigeni magoti tu, inamisheni... Ninyi watoto, Uzao wa Ibrahimu, ambao mmefanya safari ndogo ya kilimwengu, na kushuka kwenda Misri, hatuwaombi mjiunge na kanisa hili, sasa, tunawaomba mrudi kwenye ile ahadi. Mtarudi? Rudini.

<sup>230</sup> Ninyi vijana wanawake hapa nje, mama zenu wenyewe walikuwa na tukio hilo alilozungumzia, mmemsikia wakati alipolia na kumsihi Mungu, labda mlimfuata kaburini, huyo mama atashangaa kama wewe hauko Huko, njoo sasa, hivi utakuja? Rafiki mwenye dhambi, nenda madhabahuni, usiku wa leo.

... pamoja Naye, pamoja Naye kotekote.

Nitaambatana Naye bustanini,  
Nitaambatana Naye...

Kama utaambatana Naye kupitia bustanini, kwa nini usije madhabahuni pamoja Naye?

... bustanini,  
Nitaambatana Naye bustanini,  
Nitaambatana Naye, pamoja Naye kotekote.

<sup>231</sup> Wakati mkiwa, mmeinamisha vichwa vyenu, sasa huyu kijana mwanamume, na hao wengine wamekuja madhabahuni, wakupiga magoti. Sasa, sijui ni wangapi humu ndani, kama baadhi yenu Wakristo mngali mna mzungu kwa ajili ya nafsi zilizopotea. Sasa, kama kuna wenye dhambi wengine zaidi, ama wengine zaidi wanaomtafuta Mungu, mwaweza kuja?

<sup>232</sup> Nanyi mnaovutiwa na nafsi za watu hawa sasa, ambao Roho Mtakatifu amewaleta madhabahuni, je, mtakuja? Baadhi yenu akina mama na baba, wakumbatieni watoto hawa, na mwaonyeshe ya kwamba mnawapenda, nanyi mnawataka wawe raia wa Ufalme wa Mungu. Je, mtakuja, wakati tukiimba tena, "Nitaambatana Naye kotekote"? Mtakuja mpige magoti madhabahuni?

Mwenye dhambi, njoo pamoja nao sasa; aliyerudi nyuma, njoo pamoja nao, pia. Njoo tu, upige magoti madhabahuni, tafadhali.

Nitaambatana Naye hukumuni,  
Nitaambatana Naye hukumuni,  
Nitaambatana Naye hukumuni,  
Nitaambatana Naye, pamoja Naye kotekote.

<sup>233</sup> Sasa, si kulijibu kanisa, bali ninataka tu kuwaonyesha Wakristo kile ninachomaanisha: Pamoja na wenye dhambi madhabahuni, pamoja na angalau watu mia tatu hapa

walioinua mikono yao kwamba walikuwa ni Wakristo, nami nikiwasihia watu waje madhabahuni, na yapata wawili au watatu wakaitikia. Hivi hamwoni kanisa limekufa? Hakuna shauku tena kanisani kwa ajili ya nafsi zilizopotea.

<sup>234</sup> Kama hiyo ingekuwa katika maskini Kanisa la Kimishenari la Kibaptisti huko chini Kentucky, wakati mwanamke huyo aliposimama huko nyuma kuja madhabahuni, kungekuwa na mama wazee kumi na watano ama ishirini karibu naye, wakipiga mayowe na kulia na kumshukuru Mungu kwa ajili yake. Mnaona, tumepoteza hamu yetu, tumeshikwa na baridi tukafifia, tunangojewa tu hukumu, hivyo tu, itakayomwagwa.

...hukumuni,

Nitaambatana Naye, pamoja Naye kotekote.

Na...Aniongozako nitamfuata,

Aniongozako ni...(. . . ? . . .)

Aniongozako nitamfuata,

Nitaambatana Naye, pamoja Naye kotekote.

Wakati muziki ukiendelea kucheza, hebu na tuinamishe vichwa vyetu basi kwa ajili ya maombi.

Sasa, hapo madhabahuni, wekeni mikono yenu juu ya watoto hao, juu ya watu hao. Na tuinamishe vichwa vyetu.

<sup>235</sup> Bwana Yesu, njoo, Mungu mwenye rehema, njoo upesi, Bwana. Ninaamini ya kwamba saa ziko karibu kwisha, uamsho Marekani umekwisha, tunaokota tu masazo katika mashamba ya uamsho uliozimika.

<sup>236</sup> Bwana Yesu, ninaomba ya kwamba watoto hawa wanaokuja madhabahuni usiku wa leo, kwamba Roho Mtakatifu angeweza kupata moyo mwaminifu, na kuwavuta madhabahuni. Imeandikwa katika Neno lako, “Yeye anijiaye mimi sitamtupa nje kamwe.” Mtume Roho wako Mtakatifu juu yao, Bwana. Wabariki, ninaomba, Baba. Wape ubatizo wa Roho Mtakatifu, wasamehe dhambi zao.

<sup>237</sup> Samehe makosa ya hili kanisa na ya hawa watu, tupate kuwa kanisa linalowaka moto, Bwana. Sio tu ukoo nusu wa kimadhehebu, bali mwa—mwana na binti wa Mungu waliozaliwa mara ya pili. Tujalie, Bwana. Tutumie uamsho, ama utuondoe duniani, Bwana, hilo ndilo ombi letu. Jalia uamsho uje, ama utuondoe, Baba, mioyo yetu haiwezi kuvumilia jambo hilo.

<sup>238</sup> Tutume kwenye huduma za kimishenari zinazowaka moto, ambako makumi ya maelfu wanangojewa kusikia neno moja la Yesu, ambao wangeitia giza madhabahu, wakipiga mayowe na kulia wapate rehema; na, usiku wa leo, katika nchi ya uenyeyi wetu wenyewe, wamekufa, wamekauka, wamekwisha, wameokota masazo, wamepoa, huko chini Misri, wakichukuliwa na tamaa za namna nyingi, wasiweze kujifunza kamwe, wala kuufikia ujuzi wa ile kweli.

<sup>239</sup> Baba Mungu, waokoe wale wanaoweza kuokolewa, ninaomba, ninaposhuka kwenda kuwawekea mikono. Jalia Roho Mtakatifu aje, Bwana, awaamshe hawa jamaa wadogo, katika Jina la Yesu Kristo, tunapoomba.

<sup>240</sup> Endelea kuomba, Mchungaji. Ninashuka kwenda kuwaombea. [Ndugu Branham anawaombea wale walio madhabahuni. Mchungaji anaongoza ibada—Mh.]

... pamoja Naye kote.

Aniongozako nitafuata,

Aniongozako nitafuata,

Ambapo Yeye...

Hiyo ni kweli, ewe kijana, inua mikono yako, na umwamini Yeye, umkubali. Huyu ni Roho Mtakatifu hapo pamoja nawe.

Nitaambatana Naye, pamoja Naye kotekote.

<sup>241</sup> Ni kitu gani kilichokufanya uje madhabahuni? Mungu alikuleta madhabahuni. Unaweza kufanya nini ila kuungama dhambi zako? Yeye atakayekiri dhambi zake, Mungu ni mwenye haki kuzisamehe. Mwamini Bwana Yesu Kristo sasa, mkubali kama Mwokozi wako binafsi, ujue ya kwamba Yeye anakusamehe dhambi zako.

Kijana, Bwana Yesu anakusamehe dhambi zako, kama utamkubali Yeye kama Mwokozi wako. Usingeweza kuja madhabahuni peke yako.

Mama uliyeinua mkono wako, usingeweza kuja kwa nguvu zako mwenyewe.

<sup>242</sup> Bwana, unakuja ukitubu pale, mwanamume wa kwanza kuja madhabahuni, je, unamkubali Yesu kama Mwokozi wako, na kuamini Yeye anaweza kukuondolea tabia yako, na kukufanya kiumbe kipya ndani Yake? Je, unamkubali sasa kama Mwokozi wako? Je, wewe uliyeinua mkono wako, unamkubali kama Mwokozi wako, ukiamini atakupua ubatizo wa Roho Mtakatifu?

<sup>243</sup> Je, wewe, kijana, unafanya jambo lile lile? Unamkubali kama Mwokozi wako binafsi? Inua mkono wako, useme, “Yeye ni wangu. Sasa ninamwamini Bwana Yesu Kristo.” Jambo ndilo hilo. Hiyo ndiyo njia. Jambo ndilo hilo, hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo.

<sup>244</sup> Ninyi wengine hapa madhabahuni, mnaweza kumwamini Yeye, kuamini ya kwamba Yeye anawachukua kwenye Neno Lake? Anakuchukua... Lolote unalokiri Kwake, amini ya kwamba atalifanya, Yeye ni mwenye haki na mwaminifu na yuko tayari kulifanya.

<sup>245</sup> Mnaamini hilo? Kama mnaamini, simameni kwa miguu yenu. “Yeye atakayenikiri mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.” Hiyo ni kweli. Mungu awabariki. Amina. Hayo hapo maungamo yenu. Mungu asifiwe.

(“Vita vitakapokwisha, tutavaa taji.” “Vita vitakapokwisha, tutavaa taji.”)

Basi vita vitakapokwisha, sisi . . .

Sasa njoni madhabahuni, peaneni mikono na watu hawa. Njoni huku, peaneni mikono nao.

. . . tutavaa taji,  
Basi vita vitakapokwisha, tutavaa taji  
Katika Yerusalemu Mpya.  
Kuvaa taji, kuvaa taji,  
Kuvaa taji angavu na inayometameta.  
Basi vita vitakapokwisha, tutavaa taji,  
Katika Yerusalemu mpya.

<sup>246</sup> Ninataka kuwauliza jambo fulani. Maadamu mnaona watu wakija madhabahuni, wakijipatanisha na Mungu, bado kuna matumaini kwetu. Sasa, angalieni, watu hawa wangeweza kufanya nini? “Ni kitu gani kinachoweza kuosha dhambi zangu? Hakuna ila Damu yake Yesu.” Ni kitu gani kilichowaleta madhabahuni? “Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Mungu aliwavuta. Wanaweza kufanya nini? Njoo ukakiri, “Mimi ni mwenye dhambi. Mungu unisamehe kwa ajili ya Kristo. Nitakuwa Wako, Wewe uwe wangu.” Kisha ugeukie umma, na kusema, “Ninamkubali Yesu kama Mwokozi wangu binafsi, Yeye ni wangu.”

“Yeye atakayenikiri mbele ya watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu.”

<sup>247</sup> Ninyi, usiku wa leo, mnaokuja madhabahuni mnaotaka kumkubali na kuamini, na mmemkubali, na tangu saa hii juu ya ahadi ya kwamba mtaishi kwa ajili Yake, ligeukieni kusanyiko na kuinua mikono yenu. Kila mmoja wenu aje madhabahuni, huyu kijana mwanamume, huyu msichana, chini hapa ndani, na huyo mzee, inua mkono wako, useme, “Sasa ninaamini, ninamkubali.”

<sup>248</sup> Sasa, nataka kanisa lije huku, peaneni mikono nao na kuwaambia ya kwamba mna furaha kwamba wao ni Wakristo. Njoni huku, mnaweza kufanya kiasi hicho, haitawachukua ila sekunde moja tu. Peaneni mikono na kuwaambia mna furaha, mtakuwa mkiwaombea.

Jichagulie kanisa.

Basi vita vitakapokwisha, tutavaa . . .

Utapata Ushirika, pia, vita vitakapokwisha.

. . . taji, naam, tutavaa . . .

Sasa ninairudisha ibada kwa mchungaji wenu.

. . . vita vitakapokwisha . . .

Mungu awabariki. 

61-0209 Yehova-Yire  
First Assembly Of God Of Long Beach  
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS  
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.  
[www.branham.org](http://www.branham.org)

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

[www.branham.org](http://www.branham.org)